# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**FEBRUARI, 2025**

# TABLE OF CONTENTS

**SEHEMU YA KWANZA**........................................................................................1
**1.0 UTANGULIZI**........................................................................................1
**1.2 MUUNDO WA KAMATI**........................................................................................2
**1.3 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI**........................................3
**1.4 HADIDU REJEA**........................................................................................4
**SEHEMU YA PILI**........................................................................................5
**2.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**........................................5
**2.1 MABARAZA /BODI/OFISI:**........................................................................................5
**2.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**........................................................................................5
**2.3 PROGRAMU YA ELIMU YA JUU**........................................................................................6
**2.3.1 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)**........................................7
**2.3.2 TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KARUME- PEMBA**........................9
**2.3.3 CHUO KIKUU CHA ABDULRAHMAN AL-SUMAIT**........................................10
**2.3.4 CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR (ZU)**........................................................................12
**MAFANIKIO:**........................................................................................12
**2.4 PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI**........................................13
**2.4.1 SKULI YA SEKONDARI DR. AMAN KARUME**........................................14
**2.4.2 MRADI WA UJENZI WA HOSTELI-KIWANI:.**........................................14
**2.4.3 KITUO CHA UBUNIFU WA KISAYANSI (HABS) NA SKULI YA SEKONDARI -LIMBANI**........................................................................................15
**2.4.4 MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MITIHANI-UTAANI**........................16
**2.5 PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU**........................................................................................16
**2.5.1 MRADI WA UKARABATI WA TC-BUBUBU**........................................17
**2.5.2 BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR**........................................18
**2.6 PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA**........................................19
**2.6.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Elimu Pemba**........................................21
**2.7 MAPATO NA MATUMIZI**........................................................................................21
**2.8 UPATIKANAJI NA MATUMIZI YA FEDHA**........................................22
**2.8.1 CHANGAMOTO KWA UJUMLA**........................................................................................22

**2.8.2 MAONI/USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI**........23
**SEHEMU YA TATU**........26
**3.0 WIZARA YA AFYA**........26
**3.1 IDARA:**........26
**3.1.2 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA**........26
**3.1.3 BODI ZA USIMAMIZI NA TAASISI**........27
**3.1.4 MAARAZA YA WATAALAMU NA HUDUMA ZA AFYA**........27
**3.1.5 MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA.**........28
**3.1.6 VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**........29
**3.2 PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)**........31
**3.2.1 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA CHAKE CHAKE.**........32
**3.2.2 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA UKUTINI**........33
**3.2.3 ZIARA YA KAMATI BANDARINI UNGUJA**........34
**3.2.4 UTEKELEZAJI WA MRADI WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII.**........35
**3.3 PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)**........37
**3.3.1 KITENGO CHA HUDUMA ZA DAMU SALAMA.**........38
**3.3.1 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI BINAFSI**........40
**3.3.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI ZA WILAYA.**........41
**3.4 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103)**........48
**3.4 MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF)**........49
**3.5 PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2)**........51
**3.5.1 ZIARA YA KAMATI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO.**........53
**3.5.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA AFYA KWA UJUMLA**........58
**3.5.3 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**........59
**3.6 HALI YA KIFEDHA KWA UJUMLA.**........62
**3.6.1 MAPATO**........62
**3.6.2 UPATIKANAJI NA MATUMIZI YA FEDHA**........63
**SEHEMU YA NNE**........64

**4.0 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** ........... 64
**4.1 UPATIKANAJI WA FEDHA** ........... 65
**4.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU** ........... 66
**4.3 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)** ........... 66
**4.3.1 CHANGAMOTO** ........... 66
**4.3.2 MAONI /USHAURI WA KAMATI.** ........... 67
**4.4 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)** ........... 68
**4.4.1 ZIARA YA KAMATI DAR ES SALAAM** ........... 68
**4.4.2 ZIARA YA KAMATI KATIKA SHIRIKA LA SAVE THE CHILDREN** ........... 69
**4.4.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA VIKUNDI VYA KINA MAMA VINAVOSIMAMIWA NA MRADI WA TOKOMEZA.** ........... 71
**4.5 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)** ........... 72
**4.5.1 CHANGAMOTO** ........... 72
**4.5.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI.** ........... 73
**SEHEMU YA TANO** ........... 76
**5.1 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.** ........... 76
**5.1.1 SEKTA YA HABARI** ........... 76
**5.1.2 SEKTA YA VIJANA** ........... 76
**5.1.3 SEKTA YA MICHEZO** ........... 77
**5.2 UPATIKANAJI WA FEDHA** ........... 77
**5.3 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI** ........... 78
**5.3.1 SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS)** ........... 78
**5.3.2 MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA SHIRIKA LA MAGAZETI.** ........... 79
**5.3.3 WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)** ........... 80
**5.3.5 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA RADIO ISTIQAMA PEMBA.** ........... 83
**5.4 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** ........... 83
**5.4.1 MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA SANAA** ........... 84
**5.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR** ........... 84
**5.4.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA MRADI WA UKARABATI WA UWANJA WA AMAANI NA GOMBANI AWAMU YA PILI** ........... 86

**5.4.4 MRADI WA UJENZI WA VIWANJA VYA WILAYA NA MIKOA.** ................88
**5.5 PROGARAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA (PJ0302)** ..............................90
**5.5.1 CHANGAMOTO** ......................................................................................90
**5.5.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI** .........................................................91
**5.6 PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA (PJ0304)** ..91
**5.6.1 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** ..........................................................91
**5.6.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ..................................92
**6.0 HITIMISHO** ......................................................................................................92

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni **119(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2024).**

Kazi na majukumu ya Kamati hii yameelezwa na kufafanuliwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

(a). Kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

(b). kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;

(c). Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika;

(d). Kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;

(e). Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka;

(f). Kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika;

(g). Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo; na

(h). Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika Ripoti hii inajulikana kama "Kamati" ambapo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara nne (4) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Wakala, Mabaraza na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo.

Wizara hizo ni:- (a)Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; (b)Wizara ya Afya; (c) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na (d)Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## 1.2 MUUNDO WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Chum Kombo Khamis | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| 10. | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu |
| 11. | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |

## 1.3 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:

(a) Kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2023/2024.

(b) Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2023/2024.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2023/2024.

(d) Kufanya ziara katika maeneo na taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki Sita kama ifuatavyo:

(i) Tarehe 12/08/2024 hadi tarehe 16/08/2024 kwa upande wa Dar - Es - Salam na kuanzia tarehe 16/08/2024 hadi tarehe 23/08/2024 kwa upande wa Unguja.

(ii) (ii) Tarehe 04/11/2024 hadi tarehe 08/11/2022 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 11/11/2024 hadi tarehe 15/11/2024 kwa upande wa Unguja.

(iii) (iii) Tarehe 21/01/2025 hadi tarehe 24/01/2025 Pemba na kuanzia tarehe 27/01/2025 hadi tarehe 31/01/2025 Unguja.

## 1.4 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2024/2025, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:

(a) Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2024;

(b) Taarifa Rasmi za Baraza 'Hansard' za Baraza za Mwaka **2024/2025;**

(c) Ripoti za Kamati kwa Mwaka wa fedha **2023/2024;**

(d) Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mafunzo ya Amali inaundwa na Idara Saba (7), Mabaraza Matatu (3), Bodi pamoja na Ofisi mbili (2) kama ifuatavyo:

**IDARA:** (i) Idara ya Uendeshaji na Utumishi; (ii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; (iii) Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi; (iv) Idara ya Elimu ya Sekondari; (v) Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima; (vi) Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu; (vii) Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu; na (viii) Ofisi Kuu Pemba.

### 2.1 MABARAZA /BODI/OFISI:

(i) Baraza la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia;
(ii) Baraza la Mitihani Zanzibar;
(iii) Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
(iv) Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
(v) Bodi ya Taasisi ya Elimu Zanzibar;
(vi) Bodi ya Huduma za Maktaba;
(vii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu;
(viii) Ofisi Kuu Pemba
(ix) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu

### 2.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

Mpango kazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unatekelezwa kupitia programu sita kama ifuatavyo:

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari.

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawala

Programu hizi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje.

Pamoja na Programu hizo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia inatekeleza. Miradi Mitano (3) ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ambayo ni hii ifuatayo:

(i) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu katika Elimu.

(ii) Mradi wa uimarishaji wa Elimu ya Juu.

(iii) Mradi wa uimarishaji wa Ubora wa Elimu kupitia upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, Mafunzo ya walimu na Matumizi ya TEHAMA

Kamati katika utekelezaji wa kazi zake iliweza kufuatilia utekelezaji wa Programu za Wizara kama ifuatavyo:

## 2.3 PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Programu hii ina lengo la kutoa elimu itakayomuwezesha mhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Progamu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma; ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti, Huduma ya

Sayansi na Teknolojia, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya TSh. 210,747,937,698 zimepangwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hii. Kati ya fedha hizo, Tsh.35,981,775,698 ni kwa kazi za kawaida na Tsh.174,766,162,000 kwa kazi za maendeleo.

### 2.3.1 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

i. SUZA imeweza kudahili Jumla ya wanafunzi wapya 2,326 kwa mwaka wa masomo 2024/25. Sambamba na kufanya mapitio ya programu mbali mbali ikiwemo; Shahada ya Sayansi ya Komputa, sayansi ya kilimo jumuishi, Doctor of Medicine na Dental Surgery pamoja na kukamilisha uandaaji wa Mitaala kwa ajili ya Programu za Elimu na Tehama.

ii. Aidha, Jumla ya wafanyakazi 40 walipatiwa mafunzo ya siku 5 ya usimamizi wa Miradi ya ujenzi yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Tanzania Bara.

#### 2.3.1.1 CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

(a) Kamati imebaini kuwepo kwa Kuchelewa kupatikana kwa mrejesho wa maombi ya kibali cha ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika Chuo Kikuu cha Taifa.

(b) Kuchelewa kupatikana kwa vibali vya ajira kwa wataalamu kutoka nje ambapo SUZA inakabiliwa na upungufu wa Wataalamu kwa asilimia 41.

(c) Kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi wa kuimarisha elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET).

### 2.3.1.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(i) Kamati haikuridhika kwa kuchelewa utekelezaji wa Miradi ya ujenzi kupitia Mradi wa Kuimarisha elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET), eneo ambalo linachukua zaidi ya asilimia 70 ya mradi huo. Licha ya kutekelezwa kwa maeneo mengine ya Mradi huo, eneo hilo ni muhimu na Wizara inahitaji kulisimamia ipasavyo ili kuhakikisha kuwa SUZA inakamilisha taratibu zote zinazohitajika na Miradi hiyo ya ujenzi inapata baraka zote na kuanza kutekelezwa.

(ii) Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa SUZA kwa kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa Kibali cha ajira za watumishi hasa kwa wataalamu wabobezi ili chuo hicho kiweze kwenda sambamba na upatikanaji wa elimu bora ya vyuo kwa wakati uliopo.

(iii) Kamati inapongeza SUZA kwa kuweza kudahili Jumla ya wanafunzi wapya 2,326 kwa mwaka wa masomo 2024/25. Sambamba na kufanya mapitio ya programu mbali mbali ikiwemo; Shahada ya Sayansi ya Komputa, sayansi ya kilimo jumuishi, Doctor of Medicine na Dental Surgery pamoja na kukamilisha uandaaji wa Mitaala kwa ajili ya Programu za Elimu na Tehama.

(iv) Kamati inakipongeza Chuo kikuu cha SUZA kwa kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake katika fani mbali mbali. Jumla ya wafanyakazi 17 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu nchini kwa fani za kipaumbele zikiwemo; Shahada ya uzamivu, Fedha, IT na Mawasiliano ya Umma. Aidha, wafanyakazi 40 walipatiwa mafunzo ya siku 5 ya usimamizi wa Miradi ya ujenzi yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Tanzania Bara.

### 2.3.2 TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KARUME- PEMBA

Taasisi hii ni Taasisi ya umma iliyo chini ya Wizara ya elimu na mafunzo ya amali Zanzibar ambayo ilianzishwa rasmi mwaka 1966. Tangu kuanzishwa kwake Taasisi imekuwa ikitoa elimu ya sayansi na teknolojia kwa kwangazi mbali mbali kuanzia mafunzo ya amali kupitia VTA na NACVET. Kwa sasa Taasisi inajumla ya program 15 za mafunzo ya amali, Astashahada na Shahada pamoja na mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali za Sayansi na Teknolojia.Tawi la Taasisi ya Sayansi na teknolojia Karume Pemba lilianzishwa mwaka 2024 kufuatia maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi kuifungua Pemba kiuchumi.

Jumla ya shilingi za kitanzania 110,000,000 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati huo ambapo hadi Kamati inatembelea iliarifiwa kutumika shilingi za kitanzania 97,983,000 na ujenzi kufikia asilimia 90.

#### 2.3.2.1 CHANGAMOTO

(i) Taassisi inakabiliwa na changamoto ya watumishi wakudumu Tawi la Pemba, jumla ya watumishi 28 wa fani mbali mbali wanahitajika.Hali iyopo, Taasisi imefikiria kuazima wakufunzi kutoka taasisi za serikali ili kuweza kuanzisha kozi zilizopangwa huku ikisubiri kibali cha ajira kutoka utumishi.

#### 2.3.2.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**(i)** Kamati imeridhika na hatua ya ukarabati iliyofikiwa na inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Tawi la KIST Pemba ambapo kuanzishwa kwa tawi hili kutatoa fursa kwa wakaazi wa Pemba na maeneo ya karibu kupata mafunzo ya sayansi na teknolojia .

**(ii)** Kamati inaipongeza Wizara kwa kutumia wataalamu wa ndani wa KIST katika kufanya ukarabati huo hali iliyopelekea kupunguza gharama kubwa za kazi hiyo.

**(iii)** Kamati inaishauri Wizara kuwa na mpango wa muda mrefu wa kuliendeleza eneo la kudumu la Mradi wa ujenzi wa Tawi la KIST -Wingwi kwa kuliwekea miundo mbinu ya kisasa itakayozingatia mahitaji ya kidunia ya Taaluma ya sayansi na teknolojia.

(iv) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inasimamia vizuri mapato ya Taasisi (KIST) yatokanayo na utoaji wa huduma za kitaaluma katika tawi la Pemba.

### 2.3.3 CHUO KIKUU CHA ABDULRAHMAN AL-SUMAIT

Ni miongoni mwa vyuo Vikuu Binafsi vinavyoa huduma ya elimu ya vyuo vikuu Zanzibar ambacho kimeanzishwa mwaka 2014.

#### 2.3.3.1 MAFANIKIO:

1. Kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na chuo kutoka 378 mwaka 2021/2122 na kufikia 730 kwa mwaka 2024/2025
2. Uboreshaji wa miondombinu ya chuo ikiwemo,hospitali ya kisasa na jengo jipya la Tehama
3. Chuo kupata ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kutoa huduma za kitaaluma kwa kipindi cha miaka 10 ijayo.
4. Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Chuo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika masula mbali mbali ya kitaaluma na utoaji wa huduma katika sekta ya elimu kwa ujumla.
5. Kuanzisha vitengo mbali mbali kusaidia wanafunzi katika maendeleo ya masomo; Mfano Chuo kimeweza kuanzisha Kitengo cha ushauri nasaha ili

kusaidia kukabiliana na changamoto mbali mbali za kisaikolojia kwa wanafunzi.

### 2.3.3.2 CHANGAMOTO

1. Kuchelewa kupatiwa huduma ya Bima ya Afya ya Zanzibar (ZHSF) kwa wanafunzi. Sambamba na kuongezeka kwa gharama za huduma hiyo kutoka shilingi 50,400 waliyokua wakilipia katika Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) hadi kufikia shilingi 60,000 kwa huduma ya Bima ya Afya ya Zanzibar (ZHSF).
2. Uhaba wa madarasa kufuatia ongezeko kubwa la wanafunzi
3. Upungufu wa wataalamu wakiwemo walimu wa fani ya lugha fasaha ya uandishi wa lugha ya Kiswahili.
4. Makato ya Bima ya Afya ya ZHSF kwa wafanyakazi yanayofanyika kutoa katika "Gross salary" badala ya "Basic Salary" kama inavyofanyika kwa wafanyakazi wa taasisi za umma au Serikali.

### 2.3.3.3 MAONI/USHAURI MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kuvisimamia vizuri vyuo Vikuu binafsi katika kuhakikisha kuwa vyuo hivyo vinafanya vizuri kwa mujibu wa miongozo ya kitaaluma iliyopo katika utoaji wa elimu katika Vyuo hivyo.
2. Kamati inakipongeza chuo kwa maendeleo yaliyofikiwa na kukiwezesha Chuo kupata ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kutoa huduma za kitaaluma kwa kipindi cha miaka 10 ijayo.
3. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa chuo kuwaendeleza kielimu walimu wenye sifa ya kuendelezwa ili kuondosha upungufu wa fani mbali mbali ambazo ni changamoto katika vyuo vilivyopo nchini.

4. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inasimamia kusaidia kupatiwa Bima ya Afya wanafunzi wa chuo ili iweze kuwasaidia wakati wanapokabiliwa na matatizo ya kiafya.

**2.3.4 CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR (ZU)**

**MAFANIKIO:**

(i) Kuongezeka kwa wanafunzi wanaojiunga na chuo kutoka 1806 mwaka 2020/2021 na kufikia 4192 kwa mwaka 2024/2025

(ii) Kuongezeka kwa Programu za masomo katika ngazi ya Diploma, Digirii ya kwanza, ya pili na PHD.

(iii) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Chuo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika masula mbali mbali ya kitaaluma na utoaji wa huduma katika sekta ya elimu kwa ujumla.

(iv) Kuimarika kwa mahusiano baina ya chuo, vyuo pamoja na Taasisi mbali mbali za kitaaluma za ndani na nje ya nchi.

**2.3.4.1 CHANGAMOTO:**

1. Kutozingatiwa ipasavyo ZU**,** kushirikishwa katika Miradi ya serikali ya sekta ya elimu.
2. Uhaba wa wafanyakazi
3. Kuchelewa kwa baadhi ya wakati malipo ya mikopo ya wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo Zanzibar.

**2.3.4.2 MAONI/USHAURI MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(i) Kamati imeridhika na maendeleo ya utoaji wa elimu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar **(ZU)**.

(ii) Kamati inakipongeza Chuo kwa Kuimarisha mahusiano na vyuo pamoja na Taasisi mbali mbali za kitaaluma za ndani na nje ya nchi.

(iii) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuangalia namna ya kuweza kushirikisha Vyuo vikuu binafsi katika Miradi ya serikali ya sekta ya elimu ili vyuo hivyo viweze kuchangia zaidi maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

(iv) Kamati inaishauri wizara kuhakikisha kuwa inafuatilia miradi ya ujenzi inayoanzishwa na vyuo vikuu binafsi ili iweze kuifahamu na kutoa mashirikiano katika utekelezaji wa miradi hiyo.

(v) Kamati inaishauri Wizara kupitia Bodi ya Mikopo Zanzibar kuhakikisha kuwa inakamilisha malipo ya mikopo ya wanafunzi katika vyuo kwa wakati ili vyuo hivyo viweze kuendesha shughuli za kitaaluma kwa ufanisi.

## 2.4 PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI

Lengo la Programu hii ni kuimarisha Elimu ya Sekondari kwa kuhakikisha vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya mitihani ya taifa kwa skuli zote za Sekondari zenye kidatu cha nne, tano na sita vinanunuliwa na kusambazwa katika skuli hizo.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya TSh. 242,537,540,535 zimepangwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hii. Kati ya fedha hizo,Tsh. 111,448,040,535 ni kwa kazi za kawaida na Tsh. 131,109,500,000 kwa kazi za maendeleo.

Kamati katika ufuatiliaji utekelezaji wa Programu hii, imeweza kutembelea sehemu zifuatazo ili kufahamu changamoto na mafanikio na kuweza kuishauri Serikali:

### 2.4.1 SKULI YA SEKONDARI DR. AMAN KARUME

### 2.4.1.1 CHANGAMOTO:

i. Kukosekana kwa sehemu ya jiko
ii. Usafiri wa uhakika kwa wanafunzi hasa panapotokea dharua ya ugonjwa
iii. Upungufu mkubwa wa walimu
iv. Sehemu ya kuhifadhia huduma ya maji kwa mujibu ya wanafuzi waliopo

### 2.4.1.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(i) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inakuwa na utaratibu wa kufuatilia mara kwa mara mahitaji ya huduma za wanafunzi katika dahalia ili kufahamu matatizo yaliyopo na kutafutiwa ufumbuzi.

(ii) Kamati inaishauri Wizara kuwa na utaratibu endelevu wa kukaa na wazee kueleza maelekezo ya Serikali kuhusu uchangiaji wa wanafunzi katika baadhi ya huduma za elimu.

**2.4.2 MRADI WA UJENZI WA HOSTELI-KIWANI:** Ni mradi unaogharimu zaidi ya Tz Shilingi Bilioni 1.25 ambao utakuwa na majengo mawili kwa ajili ya wanafunzi 288 wanawake na wanaume.

### 2.4.2.1 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(i) Kamati inaishauri Wizara kuzingatiwa uwekaji wa miundo mbinu wezeshi katika mradi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(ii) Kamati inashauri ujenzi utakapokamilika kuzingatiwe upandaji wa miti katika eneo hilo.

(iii) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa ujenzi unakuwa na uzio kwa ajili ya ulinzi na kuepuka eneo kuvamiwa na wahalifu.

### 2.4.3 KITUO CHA UBUNIFU WA KISAYANSI (HABS) NA SKULI YA SEKONDARI -LIMBANI

Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha ufaulu katika masomo ya sayansi.Wizara imeanzisha vituo hivi kila Wilaya ili kufanikisha lengo hilo.

#### 2.4.3.1 CHANGAMOTO

(i) kuwepo kwa wimbi kubwa la watumiaji wa kituo kutoka nje.

(ii) uhaba wa nafasi katika kituo

(iii) kutokuwepo kwa ukumbi wa mikutano na sherehe maalum

(iv) kukosekana kwa uzio kwa ajili ya ulinzi na kuepuka eneo kuvamiwa na wahalifu.

#### 2.4.3.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(i) Kamati inaipongeza wizara kwa kufikiwa kwa lengo kuu la kuanzishwa kwa Kituo ambapo ubora wa ufaulu wa wanafunzi umefikia asilimia 80.

(ii) Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikisha kituo hicho kuungwa na Mkonga wa Taifa. Hatua hiyo itasaidia kurahisisha kuondosha changamoto ya rasilimali muhimu kama walimu na vifaa katika kutoa huduma bora ya elimu ya sayansi katika vituo hivyo.

(iii) Kamati inaishauri wizara kuzingatia kuwa na Miradi ya baadae yenye Vituo vikubwa vya Ubunifu wa Kisayansi **(HABS)** vitakavyokidhi mahitaji ya jamii ya baadae katika eneo husika.

(iv) Kamati inaishauri Wizara kuyafanyia maboresho madirisha ya kituo hicho kwa kuyawekea waya ili kuepusha uharibifu wa vifaa vilivyomo katika madarasa hayo.

### 2.4.4 MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MITIHANI-UTAANI

#### 2.4.4.1 CHANGAMOTO

(i) Kuwepo kwa Upungufu wa vipoza hewa visivyokidhi ukubwa wa ukumbi.

(ii) Ukuta mdogo unaogawa ukumbi na skuli.

#### 2.4.4.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI

(i) Kamati imeridhika na Mradi wa ujenzi wa Ukumbi wa Mitihani-utaani. Ni mradi wa kiwango ambao umezingatia thamani ya fedha iliyotumika kwa ujenzi.

(ii) Kamati inaishauri Wizara kuongeza vipoza hewa ili viweze kukidhi mahitaji ya ukumbi.

(iii) Kamati inaishauri Wizara kuuongeza urefu wa ukuta ambao unaligawa eneo la Skuli pamoja na Ukumbi ili kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa utulivu bila kushughulikia shughuli nyengine zinazoendelea katika ukumbi huo.

### 2.5 PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo Moja ambayo inalenga kusimamia elimu bora katika ngazi zote za elimu na kutoa huduma za Kuandaa Mitaala na Kuratibu Uandaaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia, Kutayarisha na Kusimamia Mitihani, Ukaguzi katika ngazi ya Elimu ya Skuli na katika Mfumo wa Elimu, Kutoa Taaluma ya Habari na Mawasiliano, ili itumike kama nyenzo ya Kufundishia na Kujifunzia, Kusajili Skuli na Kutoa Leseni za Walimu, Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Kutoa fursa kwa jamii kujisomea na kutafuta taarifa za kielimu na kuibua vipaji vya michezo kwa wanafunzi. Lengo kuu la kuwepo huduma hizi ni kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu ni yenye ubora kwa manufaa ya wenye kuhitimu, jamii na Taifa kwa ujumla.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya TSh. 48,565,662,396 zimepangwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hii.Kati ya fedha hizo, Tsh. 14,920,662,396 ni kwa kazi za kawaida na Tsh. 33,645,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Kamati katika ufuatiliaji wa Programu hii, imeweza kutembelea sehemu zifuatazo ili kufahamu changamoto na mafanikio na kuweza kuishauri Serikali:

### 2.5.1 MRADI WA UKARABATI WA TC-BUBUBU

#### 2.5.1.1 CHANGAMOTO

**1.** Uhaba wa nafasi unaopelekea walimu na wanafunzi kutumia eneo moja

2. Uhaba wa vifaa mbali mbali vya kujifunzia walimu

3. Uchakavu wa kituo cha TC Bububu

#### 2.5.1.2 MAONI/USHAURI/MAPENDEKEZO KAMATI

**1.** Kamati inaishauri Wizara kuimarisha ziara za kimafunzo katika Pilot Area Dodoma ili walimu waweze kupata na kuongeza ujuzi na uzoefu na kuweza kutoa elimu bora inayozingatia maadili ya kitaaluma katika kada ya Ualimu.

2. Kamati inaishauri Wizara kujenga upya Kituo cha TC Bububu ili walimu waweze kupata elimu katika mazingira yanayoridhisha.

3. Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia **TC** kuwa na utaratibu wa kudumu wa kuweka Data Base ya kutunzia kumbukumbu za walimu ili kuwa na rikodi nzuri za walimu waliopata mafunzo na wanaohitaji kupatiwa mafunzo. Utaratibu huu utairahisishia Wizara kuwa na idadi inayofahamika ya walimu wanaohitaji kuendelezwa katika Kada hiyo.

### 2.5.2 BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ilianzishwa chini ya Sheria Namb. 7 ya mwaka 1993. Bodi ya Huduma za Maktaba inalenga zaidi kutoa huduma bora za Maktaba kwa jamii nzima ili kusaidia juhudi za Serikali katika kuinua kiwango cha elimu pamoja na kuleta maendeleo katika nyanja zote za maisha kwa kuweka misingi imara ya upatikanaji wa elimu na taarifa kwa umma.

Majukumu ya Bodi ya Huduma za Maktaba kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba ya mwaka 1993, Bodi ni pamoja na: (a) Kuanzisha, kukuza na kuendeleza Huduma za Maktaba katika Visiwa vya Zanzibar; (b) Kuhakikisha upatikanaji wa vitabu na machapisho mengineyo kutoka kwa waandishi mbali mbali wa ndani na nje ya Zanzibar; (c) Kuanzisha, kusimamia na kuendeleza Maktaba za Umma katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

#### 2.5.2.1 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Kamati katika mzunguko wa kazi zake ilipata fursa ya Kwenda kujifunza Tanzania Bara na kubadilishna uzoefu juu ya namna bora zaidi ya uendeshaji wa Shughuli mbali mbali za huduma za Maktaba na kuwa na ushauri kama ifuatavyo:

(i) Kamati inaishauri Wizara kuwa na Mpango maalum wenye muelekeo wa kuimarisha upatikanaji wa huduma za Maktaba kupitia mfumo wa kimtandao ili Kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ya elimu duniani.

(ii) Kamati inaishauri wizara kuzingatia Bodi ya huduma za maktaba kuwa na Chuo cha Ukutubu ili kupata wataalamu wabobezi watakaokuwa na umahiri wa mitaala mipya ya kada hiyo na kusaidia katika kutoa huduma za Maktaba nchini.

(iii) Kamati imefurahishwa na utaratibu wa uhamasishaji wa jamii katika kutoa taaluma kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba kwa kushiriki kwenye Maonesho mbali mbali pamoja na Mitandao ya Kijamii.

(iv) Kamati inaishauri wizara kuanzisha Programu maalum ya kuwatambua waandishi wa vitabu wa Zanzibar ambayo itapelekea waandishi hao kujitangaza na kazi zao kuweza kutambulika.

## 2.6 PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Programu hii ina lengo la kuhakikisha nyenzo bora zinapatikana na kutumika kwa kuimarisha utoaji na upatikanaji wa elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni; program ndogo ya Uongozi kwa Jumla, program ndogo ya Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na program ndogo ya Uratibu wa shughuli za elimu Pemba.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya TSh. 51,808,137,918 zimepangwa kutumika katika utekelezaji wa Programu hii. Kati ya fedha hizo, Tsh. 21,458,137,918 ni kwa kazi za kawaida na Tsh. 30,350,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji halisi wa Programu ni kama ifuatavyo: -

**Mipango Sera na Utafiti**; Programu ndogo hii inajukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Sera mbalimbali za sekta ya elimu pamoja na kufanya tafiti zitakazolenga kuimarisha huduma ya elimu.

Miongoni mwa Shughuli zilitekelezwa kama ifuatavyo;

(i) Kuandaliwa kwa Kitabu cha Takwimu ngazi ya Wilaya (Education District Profile 2024) kwa mwaka 2024.

(ii) Jumla ya walimu 909 (Pemba 394 na Unguja 515) wamepatiwa mafunzo ya Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Elimu (SIS) awamu ya pili kwa Skuli za Serikali za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba.

(iii) Rasimu ya Sera mpya ya Elimu imeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau kwa maoni. Sera hiyo itawasilishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu kupata ridhaa ya Serikali.

(iv) Wizara iliratibu na kusimamia uimarishaji wa miundombinu mbalimbali ya elimu ikiwemo umaliziaji wa madarasa 361 yaliyoanzishwa na wananchi, madarasa 355 mapya, dakhalia 14 na ukarabati wa skuli 150. Aidha, ujenzi wa skuli za chini 22 za Maandalizi (mbili kila wilaya), 16 za Msingi na 15 za Sekondari unaendelea katika maeneo mbali mbali. Sambamba na hilo Wizara imeanza ujenzi wa nyumba za walimu ambapo jumla ya nyumba 11 zimeanza kujengwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Nyumba hizi zitakuwa na uwezo wa kuchukuwa familia 3 kila moja.

(v) Aidha, Wizara imeendelea na zoezi la kuratibu na kusimamia ujenzi wa ofisi za Elimu za Wilaya katika Wilaya ya Kusini, Kaskazini B, na Magharibi A.

(vi) Mafunzo ya Mpango wa Mageuzi ya sekta ya Elimu (ZESTP) yametolewa kwa washiriki 2,553 wakiwemo Walimu wakuu, Walimu wa taaluma na wajumbe wa kamati za Skuli, Maafisa Elimu Wilaya na Wakaguzi wa elimu Wilaya na Mikoa.

(vii) Jumla ya maafisa tisa walijengewa uwezo katika maeneo mbalimbali yakiwemo Ufuatiliaji na Tathmini (3), Fedha na Mipango (3), mafunzo ya lugha ya kupokea wageni (1) na kuandaa bajeti

**Uongozi kwa Ujumla**; Programu ndogo hii inahusika na masuala yote ya Kiutumishi na Uendeshaji, kusimamia Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali

zikiwemo haki na wajibu wa Watumishi. Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipanga bajeti ya TZS 14,923,918,609 kwa robo ya pili ambapo hadi kufikia Disemba, 2024 jumla ya TZS 5,359,036,630 zilipatikana sawa na asilimia 36. Wizara kupitia Idara hii ilifanikiwa kutekeleza shughuli mbali mbali ikiwa pamoja na kuendelea na zoezi la ajira ambapo jumla ya walimu 737 wameweza kuajiriwa.

### 2.6.1 Programu ndogo ya Uratibu wa Elimu Pemba

Katika utekelezaji wa Programu ndogo hii kazi mbali mbali zilifanyika ikiwemo; Vikao 09 vilivyowashirikisha wakandarasi (KMKM, SINIC, JKU, MWINYI CO NA UNITED RAM) kwa lengo la kujadili maendeleo ya Miradi ya ujenzi wa Skuli mpya zinazoendelea kujengwa na kukarabatiwa.

## 2.7 MAPATO NA MATUMIZI

**MAPATO**

Wizara imekadiria kukusanya Jumla ya TZS. 1,140,703,000 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Mapato hayo yanatokana na vyanzo vikuu ambayo ni usajili wa skuli binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na ada za wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya taifa pamoja na usajili wa vituo vya mitihani.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya Jumla ya Tsh. 269,480,000/- ambapo hadi kufikia Disemba 2024 jumla ya Tsh. 177,812,530/- sawa na asilimia 66 zimekusanywa.

## 2.8 UPATIKANAJI NA MATUMIZI YA FEDHA

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilipanga kutumia jumla ya TZS 524,535,083,554 kwa kipindi cha mwazi July – Disemba 2024. Kati ya hizo TZS 356,186,954,708.50 ni fedha za maendeleo na (TZS 103,699,585,840 za Muhsani na TZS 103,699,585,840 za SMZ), mishahara na ruzuku ni TZS 150,293,305,809.07 na matumizi mengineyo ni TZS 18,054,823,036. Hadi kufikia Disemba 31,2024 Jumla TZS 231,386,424,813 sawa na asilimia 44 zimepatikana. Kati hizo TZS 86,743,030,897.57 sawa asilimia 43 ni fedha za maendeleo (TZS 71,483,693,010 sawa na asilimia 28 za SMZ na TZS 15,259,337,888 sawa na asilimia 15 kutoka kwa wahisani), mishahara na ruzuku 137,582,742,620.00 sawa na asilimia 92 na matumizi mengineyo ni TZS 7,060,651,295 sawa na asilimia 39.

### 2.8.1 CHANGAMOTO KWA UJUMLA

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya elimu kwa ujumla, bado Wizara inakabiliwa na Changamoto zifuatazo: -

(i) Kuwepo kwa uhaba wa vifaa vya kielektroniki katika Idara na Taasisi mbali mbali. Vifaa hivyo vinajumuisha kompyuta, printer na fotokopi.

(ii) Uchelewaji wa uingizaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati hali inayochangia ucheleweshaji katika ukamilishaji wa miradi hasa kazi ya ukarabati wa Skuli.

(iii) Kuchelewa kuanza kwa shifti moja katika skuli zetu kutokana na baadhi ya wakandarasi kushindwa kukamilisha ujenzi wa skuli na madarasa kwa wakati.

(iv) Ukosefu wa gari kwa Idara na Taasisi mbalimbali za Wizara pamoja na upungufu wa vyombo vyengine vya usafiri kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji kwa maeneo ya Mjini na Vijijini.

(v) Ukosefu wa majengo ya ofisi kwa baadhi ya Taasisi za Wizara kama vile TEZ, BMWEJ, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Idara ya Michezo na Utamaduni pamoja na Bodi ya Mikopo.

(vi) Upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi ya lazima na fedha za matumizi mengineyo zikiwemo za Ruzuku za Uendeshaji wa Skuli kulinganisha na bajeti inayoidhinishwa kwa mwaka. Hali hii inapelekea kukwama kwa baadhi ya shughuli muhimu zilizopangwa.

(vii) Baraza la Mitihani la Zanzibar linakabiliwa na Changamoto ya ukosefu wa mashine ya Uchapishaji wa Mitihani na vyeti vya wahitimu, sehemu ya kuhifadhia pamoja na sehemu ya kusahihishia mitihani.

(viii) Uhaba wa wafanyakazi katika Taasisi na Idara mbali mbali. Kama vile Taasisi ya Elimu Zanzibar na Baraza la Elimu Zanzibar.

### 2.8.2 MAONI/USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI

(i) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo jipya la Wizara ambalo litapelekea kuwa na Ofisi zake za kudumu na kufanya kazi kwa ufanisi. Haivyo Kamati inaishauri Wizara kuharakisha taratibu zote ili mradi uweze kuanza haraka na kukamilika kwa wakati.

(ii) Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuingizia fedha kwa wakati zikiwemo fedha za Ruzuku, Uendeshaji wa Skuli kulingana na bajeti inayoidhinishwa kwa mwaka. Hali hii itapelekea kukamilika kwa wakati kwa baadhi ya shughuli muhimu zilizopangwa.

(iii) Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya muda mrefu ya usafiri katika Idara na Taasisi mbali mbali za Wizara, hali ambayo

inapunguza ufanisi katika kazi za ufuatiliaji wa upatikanaji wa huduma za kielimu katika maeneo ya Mjini na Vijijini. Kamati inaisisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuwa na mpango maalum na kutoa vipaumbele katika upatikanaji wa huduma za usafiri (gari) katika taasisi za wizara.

(iv) Kamati inaishauri Wizara kutokana na kuimarika kwa Mfumo wa Sayansi na Teknologia katika sekta ya elimu ipo haja kwa Wizara kupanua wigo wa kuimarisha vyanzo vyake vya mapato vitakavyozingatia mchango na maendeleo ya mfumo huo katika sekta ya elimu nchini.

(v) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuwajengea uwezo walimu 909 kwa kuwapatia mafunzo ya Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Elimu kwa Skuli za Serikali za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba. Hatua hiyo ni nzuri na itasadia kupatikana kwa Takwimu sahihi za elimu ,hata hivyo ni vyema kwa Wizara kutoa mafunzo hayo kwa upande wa Skuli binafsi ili serikali iweze kupata uwiano wa takwimu hizo kwa usahihi na kutumika katika kuleta maendeleo katika sekta ya elimu nchini .

(vi) Kamati imeridhika na hatua iliyofikiwa Rasimu ya Sera mpya ya Elimu Zanzibar.Hata hivyo kamati inaishauri Wizara kukamilisha hatua zilizobaki ili Sera hiyo iweze kupata ridhaa ya Serikali na kuweza kutumika sambamba na Sera mpya ya Elimu ya SMT ambayo tayari imezinduliwa rasmi hivi karibuni.

(vii) Kamati inaipongeza Wizara kupitia Baraza la Mitihani kwa kusimamia ufanyaji, usahihishaji na Kutoa Matokeo mazuri ya Mitihani ya Darasa la Nne yenye asilimia ya ufaulu 94.1, asilimia 96.7 kwa ufaulu wa darasa la Saba na asilimia 84.4 kwa Kidatu cha Pili. Hata hivyo, Kamati inaishauri wizara kuzingatia kupatikana kwa Mtambo wa kisasa wa uchapishaji wa

mitihani ili baraza liweze kujitegemea kufanya shughuli zake na kuepuka gharama kutoka nje.

(viii) Kamati inaunga mkono juhudi za Wizara katika kuratibu na kusimamia vizuri uimarishaji wa miundombinu mbali mbali ya elimu ikiwemo umaliziaji wa madarasa 361 yaliyoanzishwa na wananchi, madarasa 355 mapya, dakhalia 14 na ukarabati wa skuli 150. Aidha, ujenzi wa skuli za chini22 za Maandalizi (mbili kila wilaya), 16 za Msingi na 15 za Sekondari unaendelea katika maeneo mbali mbali. Sambamba na hilo Wizara imeanza ujenzi wa nyumba za walimu ambapo jumla ya nyumba 11 zimeanza kujengwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba pamoja na zoezi la kuratibu na kusimamia ujenzi wa ofisi za Elimu za Wilaya katika Wilaya ya Kusini, Kaskazini B, na Magharibi A.

(ix) Kamati inaipongeza Wizara kwa kutoa Mafunzo ya Mpango wa Mageuzi ya sekta ya Elimu (ZESTP) kwa washiriki 2,553 wakiwemo Walimu wakuu, Walimu wa taaluma na wajumbe wa kamati za Skuli, Maafisa Elimu Wilaya na Wakaguzi wa elimu Wilaya na Mikoa. Mafunzo hayo yatawezesha walengwa kufahamu Mpango wa mageuzi ya elimu nchini na kuutekeleza kwa ufanisi.

(x) Kamati inaishauri Wizara kusimamia ipasavyo muongozo wa kazi Nambari 4 wa mwaka 2021 na Kanuni za uendeshaji wa michezo na utamaduni katika skuli kwa lengo la kuondoa changamoto za uendeshaji na usimamizi wa michezo na kurejesha hadhi ya Michezo maskulini.

## SEHEMU YA TATU

# 3.0 WIZARA YA AFYA

Wizara inatekeleza malengo yake kupitia Mfumo wa Bajeti wa Kiprogramu (PBB) ambapo ina mafungu Mawili:-

a. Fungu H01: Wizara ya Afya, ambalo lina Program kuu 3 na Programu ndogo 7

b. Fungu HO2: Hospitali ya Mnazi Mmoja ambalo lina programu kuu 2 na Programu ndogo 3.

Wizara inaundwa na Idara sita (6), Taasisi zinazojitegemea sita (6) pamoja na bodi zake, Mabaraza ya wataalamu na Ofisi kuu Pemba kama ifuatavyo:

### 3.1 IDARA:

*(i)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi;

*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

*(iii)* Idara ya Kinga na Elimu ya Afya;

*(iv)* Idara ya Tiba;

*(v)* Idara ya Uuguzi na Ukinga;

*(vi)* Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali;

*(vii)* Ofisi kuu - Pemba

### 3.1.2 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

*(i)* Hospitali ya Mnazi Mmoja;

*(ii)* Mfuko wa huduma za Afya Zanzibar;

*(iii)* Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;

*(iv)* Taasisi ya Utafiti wa Afya

*(v)* Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

*(vi)* Wakala wa Bohari kuu ya Dawa; na

### 3.1.3 BODI ZA USIMAMIZI NA TAASISI

*(i)* Bodi ya Ushauri ya Hospitali ya Mnazi Mmoja;

*(ii)* Bodi ya Ushauri ya Mfuko wa Huduma za Afya;

*(iii)* Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;

*(iv)* Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Afya;

*(v)* Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

*(vi)* Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa;

### 3.1.4 MAARAZA YA WATAALAMU NA HUDUMA ZA AFYA

*(i)* Baraza la Madaktari;

*(ii)* Baraza la Wauguzi na Wakunga;

*(iii)* Baraza la Wataalamu wa Maabara za Tiba;

*(iv)* Baraza la Wataalamu wa Afya ya Jamii na Mazingira;

*(v)* Baraza la Ushauri ya Afya ya Jamii na Mazingira;

*(vi)* Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi;

*(vii)* Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala;

### 3.1.5 MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA.

Wizara ya Afya imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Wizara yya Afya inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo 2021-2026, Dira ya maendeleo ya Zanzibar 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025, Mipango na Mikakati ya Kikanda na Kitaifa ikiwemo Agenda ya Afrika 2063 na Agenda ya Afya kwa wote ifikao 2030.

Wizara ina jukumu la kutoa huduma bora za Afya kwa wananchi wote kama ifuatavyo:-

1. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara;
2. Kushajihisha kufanya Tafiti za Afya kwa kupelekea aendeleo ya Sekta;
3. Kusimamia Uongozi, Rasilimali Watu, Fedha na Rasilimali nyengine;
4. Kusimamia utoaji wa Huduma za Afya.
5. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na miundombinu bora ya utoaji wa huduma;
6. Kuhakikisha upatikanaji wa Madaktari Bingwa na Wataalamuwengine katika ngazi zote;
7. Kusimamia na kushajihisha Elimu ya Afya ya jamii dhidi ya kinga ya maradhi mbalimbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza;
8. Kuhakikisha Chakula, Dawa na Vipodozi vinavotumika zanzibar vipo katika hali ya ubora na salama kwa matumizi ya Binaadamu;
9. Kufanya uchunguzi na kuishauri serikali juu ya matokeo ya uchunguzi wa Sampuli za sumu, madawa ya kulevya, vinasaba, miripuko na kemikali;
10. Kusimamia utoaji wa Huduma za mfuko wa Afya; na
11. Kupokea malalamiko ya Jamii na kufanyia kazi.

### 3.1.6 VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Wizara ya afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejipangia kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

a) Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri;

b) Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na vitendanishi;

c) Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya;

d) Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

e) Kuimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za afya ikiwemo mfuko wa afya Zanzibar;

f) Kuimarisha huduma za afya ya msingi kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

g) Kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka vifo **145** kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwa 2023/2024 kufika vifo **123** kwa kila vizazi hai 100,000 (Zanzibar Vision 2050) na kufikia vifo 70 kwa kwa kila vizazi hai 100,000 (SDG-2030) ifikapo 2030.

h) Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 28 kwa kila vizazi hai 1000 na kufikia vifo 26 kwa kila vizazi hai 1000 (Zanzibar Vision 2050) na hadi kufikia vifo 12 kwa kila vizazi hai 1000 (SDG-2030) ifikapo 2030;

i) Kuimarisha uwezo na utayari wa kukabiliana na majanga ya mripuko na matukio mengine ya kiafya;

j) Kuendeleza mapambano ya maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza; na Kuongeza idadi ya tafiti za afya kwa kuzingatia ajenda za nchi na kufanya uchambuzi wa tafiti hizo kwa lengo kutunga sera na miongozo ili kuimarisha huduma.

Kamati katika utekelezaji wa kazi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ilifatilia utekelezaji wa Bajeti inayotumia Programmu ambapo Wizara ilipanga kutekeleza programu zifuatazo:

**a) FUNGU H01: WIZARA YA AFYA**

*(i)* Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya;

*(ii)* Programu Kuu ya Huduma za Tiba; na

*(iii)* Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara;

**b) FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**

I. Programu Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.
II. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Wizara inatekeleza Programu hizo kupitia taasisi zake zilizoainishwa hapo juu. Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio na changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa Programu hizo ili kuishauri Serikali namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto hizo.

## 3.2 PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

Jukumu la Programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa kwa njia mbali mbali za kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza.

Katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa kupitia programu ya Kinga na Elimu ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imetenga jumla ya Shilingi **100,619,301,000/=** ambazo ni sawa na asilimia **36** ya bajeti ya Wizara kwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;
ii. Kuendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini
iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto;
iv. Kuimarisha huduma za afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege);
v. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika vituo vya afya, hospitali, maskulini na jamii;
vi. Kuendelea na mikakati ya kupambana na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza;
vii. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;
viii. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zitakazotoa matokeo ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;
ix. Kuimarisha program za uhamasishaji na kutoa huduma za afya katika ngazi zote; na
x. Kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

Utekelezaji halisi wa Programu hii ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA CHAKE CHAKE.

Kituo cha Afya cha Chake Chake ni miongoni mwa vituo vya majaribio (Pilot) kwa mfumo wa kuhudumia wagonjwa (ZanEMR) ambapo kamati ilipata fursa kukitembelea kituo hicho ili kujionea maendeleo ya mradi pamoja na kujionea utendeaji kazi wa kituo kwa ujumla wake.

#### 3.2.1.1 CHANGAMOTO:

- Kutokuwepo kwa mpango endelevu wa mfumo wa ZanEMR.
- Upungufu wa wafanyakazi wakiwemo wataalamu wa Tehama wenye sifa za kuhudumia Mfumo huo. Hali hiyo imesababisha mifumo kutosomana baina mfumo mama wa Wizara na Mfumo wa ZanEMR pamoja na Mifumo ya Hospitali moja na Hospitali nyengine.
- Kukosekana kwa intaneti ya Uhakika na yenye kasi ambayo itakua na uwezo wa kufanya kazi kwa ajili ya mifumo.
- Upungufu wa fedha za kuendeshea mradi kutokana kuongezeka kwa vituo vya majaribio (Pilot) wakati mwanzoni havikuwemo.

#### 3.4.1.2 USHAURI /MAONI YA KAMATI

i. Kamati inaishauri Wizara kuwashirikisha waalamu husika wa miradi ili kuwapatia ushauri juu ya kuiendesha miradi kabla ya miradi hiyo kuanza. Hali hiyo itapelekea miradi hiyo kufikia lengo na kuwa endelevu hasa wakati Washirika wa Maendeleo wanapomaliza muda wao wa kuihudumia miradi hiyo kwa mujibu wa Mikata husiaka.

ii. Kamati inaishauri Wizara Afya kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Sheria, Utumishi na Utwala Bora kufanya mchakato wa uajiri ili

kutatua changamoto ya uhaba wa wataalamu wa Tehama katika mifumo ambayo inaboreshwa ili iweze kutoa huduma bora za Afya.

iii. Kamati inashauri na kupendekeza kwa Serikali kupitia Wakala wa Mkonga wa Mawasiliano (ZICTIA) kuimarisha huduma ya mtandao katika vituo vyote vya afya pamoja na hospitali kwa ajili ya kurahisisha utumaji wa taarifa muhimu za afya zikiwemo za matumizi na maombi ya dawa.

iv. Kamati inashauri Wizara ya Afya kuhakikisha wanatumia vizuri fedha za miradi ili waweze kukamilisha miradi hiyo kwa wakati uliopangwa.

### 3.2.2 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA UKUTINI

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programuu hii, Kamati ilifanya ziara katika Kituo cha Afya cha Ukutini Kusini Pemba ambacho miongoni mwa majukumu yake ni kutoa huduma za clinik kwa mama wajawazito na kutoa huduma za nje (OPD). Kituo kina jumla ya Wafanyakazi 4 ambapo wuguzi wakunga 2, Muuguzi wa kawaida 1 na Muhudumu 1.

#### 3.2.2.1 CHANGAMOTO

- Kamati imebaini kuwepo kwa Ukosefu wa baadhi ya wafanyakazi wa kada mbali mbali kama Afisa Tabibu, Fundi Sanifu maabara, Fundi Sanifu Madawa na Mtaalamu wa Afya ya Mazingira.

- Kamati imebaini Kuhamishiwa kwa huduma kutoka katika kituo cha Afya na kwenda katika nyumba ya daktari.

- Ufinyu wa jengo la kutolea huduma.

- Uchakavu wa miundombinu ikiwemo jengo la kituo.

### 3.2.2.2 USHAURI /MAONI YA KAMATI

i. Kamati inashauri Wizara katika Mpango wa kuviimarisha vituo vya afya kuhakikisha kuwa wanakiimarisha kituo hiki kwa kukifanyia ukarabati mkubwa ili kurejesha huduma za matibabu kituoni hapo kama awali.
ii. Kamati inaishauri wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Shreia, utumishi na Utawala Bora kuwaongezea wataalamu kwa kada ambazo zina mapungufu ili kuengeza ufanisi katika utoaji wa huduma bora za Afya.
iii. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili waweze kuwa na muitiko wa hiari wa kwenda katika kituo cha Afya pale panapohitajika, kwa mfano; kuhudhuria Cliniki kwa Baba na Mama mwanzoni mwa kuanza cliniki kwa mama mjamzito.

### 3.2.3 ZIARA YA KAMATI BANDARINI UNGUJA

Katika udhibiti wa maeneo ya mipakani Wizara imeweka mikakati ya kuvikagua vyombo vya usafiri vya Anga na Baharini pamoja na abiria wake.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Bandari kuu ya Zanzibar kwa lengo la kupata elimu juu ya Afya katika Bandari na kujua changamoto zilizopo ili kuweza kutoa ushauri ya jinsi ya kuweza kuzitatua.

### 3.2.3.1 CHANGAMOTO

- Eneo dogo la Ofisi ambalo linatumika kwa kutolea huduma za Afya Bandarini.
- Wafanyakazi wachache ambao wanashindwa kuhudumia kundi kubwa la abiria na kwenda kukagua vyombo kwa wakati mmoja Bandarini hapo.

- Wafanyakazi Kukosa posho la ziada kwa wale wanaoingia zamu za Usiku na siku za mapumziko.
- Kukosa vitendea kazi vya kisasa katika utekelezaji wa majukumu yao.

### 3.2.3.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

I. Kamati inaishauri Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuwapatia maposho ya muda wa ziada hasa kwa nyakati za usiku na siku za mapumziko ili kuwajengea hamasa ya kiutendaji wafanyakazi wake wanaofanya kazi muda huo.

II. Kamati inaishauri Wizara ifanye mazungumzo na Wizara husika pamoja na Mamlaka ya Bandari ili kuwapatia eneo litakalokidhi kwa ajili ya mahitaji ya kazi za utoaji wa huduma za afya Bandarini.

III. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuwapatia vifaa vya kisasa wafanyakazi wa ofisi iliyopo Bandarini sambamba na kuwaongeza nguvu kazi ili waweze kutoa huduma salama za Afya kwa Raia pamoja na vyombo vya usafiri kwa kuvifanyia uchunguzi wa kitaalamu hasa vyombo vya usafiri kutoka nje ya nchi na kutoa ushauri wa kitaalamu pale panapostahiki.

IV. Kamati inaishauri Wizara kufanya mazungumzo na mamlaka inayoshughulikia Ukumbi mashuhuri (VIP) kuweza kuufanyia maboresho ili uwendane na hadhi ya watumiaji wa ukumbi huo.

### 3.2.4 UTEKELEZAJI WA MRADI WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII.

Katika kuhakikisha Afya bora kwa Wazanzibari wote, Wizara ya Afya imeanzisha mpango maalumu wa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii ili kusogeza huduma karibu kwa jamii na waweze kupata elimu sahihi juu ya kujikinga na magonjwa mbali

mbali, kugundua dalili hatarishi za magonjwa na kuwaunganisha wenye dalili hizo kwenye vituo vya Afya kwa matibabu na huduma sahihi. \

### 3.2.4.1 CHANGAMOTO

- Kukosa mashirikiano kwa baadhi ya wanajamii.
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa watoa huduma.
- Mfumo wa ukusanyaji taarifa haupo sawa.
- Kukosekana kwa kiunganishi baina ya watoa huduma na Wizara.
- Kukosa mashirikiano kwa baadhi ya Masheha

### 3.2.4.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inapongeza jitihada za serikali kupitia Wizara kwa kuweka mkakti maalum ili kuweza kutoa huduma bora za Afya mjini na vijini kwa kuweza kuanzisha Mradi huu wa huduma za Afya ngazi ya Jamii (CHW)

ii. Kamati inaishauri Wizara kukaa na masheha ili kuandaa mkakati ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwapatia mashirikiano wahudumu hawa kwa maslahi ya Afya bora kwa wananchi wote wa Zanzibar, sambamba na kupunguza wimbi la vifo vya watoto wachanga ambao sababu kubwa ni kukosa elimu kwa kina mama wajawazito juu ya athari za kujifungulia Majumbani.

iii. Kamati inaishauri Wizara kuweka Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwanunualia vitendea kazi wahudumu wetu ambao watasaidia kujua afya za wananchi kabla ya kwenda katika vituo vya afya kama vile kifaa cha kupimia presha, Sukari na vyenginevyo.

iv. Kamati inashauri Wizara kupitia waalamu wake wa Tehama kuhakikisha mifumo yote ya ukusanyaji taarifa inasomana ili kurahisisha utendaji kazi katika mradi huu pamoja na kuondoa changamoto ya malipo zinazojitokeza.

v. Kamati inaishauri Wizara kuweka muwakilishi wa CHW ambaye anatokana na wahudumu hawa ili iwe rahisi kwao kumfikia kila mdau na kufanya mawasiliano na Wizara kwa niaba ya wahumu wote.

vi. Katika kuboresha huduma zitolewazo na wahudumu wa Afya kwa ngazi ya jamii, Kamati inaona ipo haja kwa wahudumu wa kike kupatiwa mafunzo ya ukunga ili kuweza kutatua changamoto za baadhi ya mama wajawazito ambao kwa bahati mbaya wamekuwa wakijifungua majumbani au kabla kufika katika kituo cha Afya.

## 3.3 PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)

Katika kuhakikisha kwamba huduma za uchunguzi na matibabu zinaimarika zaidi, Wizara imetenga Shilingi **142,253,383,000/=** sawa na asilimia **50** ya Bageti kati ya hizo Shilingi **136,331,183,000/=** kwa ajili ya program ya matibabu na Shilingi **5,922,200,000/=** kwa ajili ya program ya Uchunguzi .

Miongoni mwa Shughuli zilopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo: -

I. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa;

II. Kutekeleza mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;

III. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa;

IV. Kuongeza ukusanyaji wa damu uniti **25,000** kwa mwaka kutoka uniti **20,000**;

V. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa, tiba na vitendanishi;

VI. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na rediolojia);

VII. Kuimarisha huduma za tiba kwa mashirikiano na sekta binafsi.

Kamati iliweza kufuatilia utekelezaji wa Programu hii katika taasisi kama ifuatavyo:-

### 3.3.1 KITENGO CHA HUDUMA ZA DAMU SALAMA.

Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Zanzibar ni Moja kati ya Muhimili Muhimu katika Wizara ya afya, Zanzibar. Mpango huu unaendeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Wizara ya Afya Zanzibar, ambapo pia unapata ufadhili kutoka Serikali ya Marekani kupitia mradi wa Afya Kamilifu AMREF.

Lengo la kuwepo mpango huu ni kuhakikisha upatikanaji wa Damu Salama ya kutosha kutoka kwa wachangiaji wa hiari, ambayo itapatikana kwa urahisi mara tu inapohitajika katika hospitali zote zinazotoa tiba ya damu Unguja na Pemba.

#### 3.3.1.1 CHANGAMOTO.

- Upungufu wa wafanyakazi hasa wa eneo la uchangiaji wa damu (Nurse and Counselors) hali inayopelekea wafanyakazi kufanyakazi hadi baada ya saa za kazi na siku za mapumziko pamoja na sikukuu ambayo inaongeza gharama za uendeshaji na kukosa muda wa mapumziko kwa wafanyakazi;
- Kukosekana kwa mfumo wenye kukidhi mahitaji wa kukusanyia Taarifa za wachangiaji Damu;
- Uchakavu wa magari kwa ajili ya shughuli za ukusanyaji Damu; na
- Uchakavu wa majengo na uhaba wa samani.

### 3.3.1.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inashauri Wizara ya Afya kuomba kibali Katika Wizara ya Utumishi ili waweze kujaza nafasi ambazo zipo pungufu katikia kitengo hiki kwa lengo la kutimiza malengo ya Serikali juu ya kuboresha huduma bora za Afya kwa wananchi wake hasa katika upatikanaji wa damu salama.

ii. Kamati inaishauri Wizara kupitia wataalamu wake wa Tehama kuhakikisha wanarekebisha mifumo yote ili taarifa za wachangiaji damu na taarifa nyengine zote zinazohusiana na kitengo hiki ziwe zinasomana.

iii. Kamati inaishauri Wizara ya Afya katika mgao wa magari ambayo watakayopatiwa kutoka Wizara ya Fedha waweze kuwapatia kitengo hiki cha Huduma ya Damu salama ili waweze kuondokana na changamoto wanayokabiliana nayo ya usafiri.

iv. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kulifanyia maboresho jengo ambalo linatumika kwa ajili ya shughuli za Huduma ya Damu Salama kwani Jengo hilo ni chakavukwa baadhi ya damu.

v. Kamati inaishauri wizara kupitia kitengo chake cha habari kutoa elimu pamoja na hamasa kwa jamii juu ya umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari ili kuondokana na tatizo la upungufu wa damu hususan kwa upande wa Unguja. Ambapo kamati imebaini kuwa utayari wa wachangiaji kwa upande wa Unguja upo chini sana ukilinganishwa na Utayari wachangiaji wa Pemba.

### 3.3.1 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI BINAFSI

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilipata fursa ya kuzitembelea Hospital Binafsi kwa lengo la kuhakikisha wanatoa huduma zilizo bora kwa wateja wao kama lengo la Serikali ya awamu ya Nane inavolitekeleza kwa vitendo katika kujali afya za Raia wake pia na kujua changamoto za Hospitali Binafsi ili kuweza kuwapa ushauri wa kuzitatua.

Kamati ilitembelea **Hospital ya Tawwakal** pamoja **Hospitali ya Arrahma** kwa upande wa Unguja na **Hospitali ya Ammal** kwa upande wa Pemba.

### 3.3.2.1 CHANGAMOTO

- ✓ Ubovu wa Barabara ambayo inatumiwa na wagonjwa wanaokwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Tawakal.
- ✓ Upatikanaji wa wateja katika hospitali ya Ammal ni mdogo kutokana na kipato cha walio wengi.
- ✓ Wataalamu wazawa kutaka kulipwa zaidi ya kile ambacho wanastahili.
- ✓ Mabadiliko ya bei kwa mfuko wa bima ya Afya NHIF umepelekea kuwa changamoto kubwa hususan katika manunuzi ya dawa.
- ✓ Kuchelewa malipo ya Bima jambo ambalo linazoretesha ufanisi wa Hospitali binafsi.
- ✓ Mfuko wa Bima ya Afya ya Zanzibar (ZHSF) kutoruhusu kupokea wagonjwa wa kawaida mpaka wapate rufaa.

### 3.3.2.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inazishukuru Hospitali Binafsi kwa kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za Afya kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma Hospitalini kwao yakiwemo matibabu ya kibingwa na Huduma za mama na Mtoto.

ii. Kamati inaishauri wizara kuweka mikakati mizuri kwa Hospital na vituo vya

Afya vya Serikali na Binafsi ili huduma za mama na mtoto ziweze kutolewa na wataalamu wanawake wenziwao tu.

iii. Kamati inaishauri Wizara iwe na utamaduni wa kukaa vikao vya mara kwa mara na Wamiliki wa Hospital Binafsi ili kuendana na Maboresho ya Wizara yaliyopo ya utoaji huduma bora za Afya nchini kama vile Upatikanaji wa dawa kutoka Bohari kuu ya Dawa na vipi wanaweza kushirikiana kwa pamoja ili kutatua chngamoto zinazojitokeza kama vile upatikanaji wa Damu salama.

iv. Kamati inaishauri wizara kuangalia namna bora ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza baina ya Mfuko wa Bima ya Afya na Hospital Binafsi hasa katika suala la ucheleweshwaji wa Malipo pamoja suala la kupokea wagonjwa kwa rufaa tu.

v. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara husika kuweza kuelekezana ni jinsi gani wanaweza kutatua changamoto ya Barabara inayoelekea Hospitalini kwao kwani inakua ni changamoto kubwa kwa wagonjwa hasa kipindi cha mvua.

### 3.3.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI ZA WILAYA.

Katika kuboresha huduma bora za Afya kwa wananchi wa Zanzibar, Seriikali ya awamu ya nane imekamilisha baadhi ujenzi wa vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya kwa kila wilaya. Kamati ya Ustawi wa Jamii ilipata nafasi ya kufanya ziara katika Hospitali za Wilaya 5 kwa Unguja na Pemba ili kujionea utendaji kazi wa Hospitali hizo pamoja na maendeleo ya miradi hiyo:-

### 3.3.3.1 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI YA KINYASINI WILAYA YA WETE.

### 3.3.3.1.1 CHANGAMOTO.

- ✓ Ukosefu wa Intaneti yenye kasi jambo ambalo linapelekea msongamano wa wagonjwa na kuchukua muda mkubwa kwenye kupatiwa huduma za kimatibabu.
- ✓ Vifaa vilioletwa vya kufanyia uchunguzi sivyo vilivokua vimeombwa.
- ✓ Uchache wa wafanyakazi wakiwemo madaktari na wauguzi.
- ✓ Ukosefu wa vitendea kazi zikiwemo computa kwa ajili ya mfumo.

### 3.3.3.1.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inaishauri Wizara kuweka mpangilio mzuri sehemu za kungojea Wagonjwa ili wazee na wenye mahitaji maalumu waweze kupewa kipaombele cha kupata huduma Hospitalini hapo.

ii. Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wakala wa Mkonga wa Mawasiliano (ZICTIA) kuimarisha huduma ya mtandao katika vituo vyote vya afya pamoja na hospitali kwa ajili ya kurahisisha utumaji wa taarifa muhimu za afya zikiwemo za matumizi ya mifumo na maombi ya dawa.

iii. Kamati imekemea vikali na kuitaka Wizara kuiagiza Kampuni iliyoleta vifaa katika **Hospitali ya Kinyasini** kinyume na makubaliano ya vifaa vilivyohitajika, yakiwemo magodoro na vifaa vyengine ambavyo vimekosa kiwango na ubora kwa matumizi kubadilishwa vifaa hivyo na kuletwa vifaa vyengine venye ubora na viwango vilivyokubalika kwa matumizi ya binadamu. Kamati inaishauri Wizara kuwasimamia ipasavyo wale wote wanaopewa dhamana ya ununuzi na wanaosambaza vifaa katika vituo vya Afya na Hospitali kuwa wanaleta vifaa vilivyo bora na vyenye kiwango .

iv. Kamati imebaini kuwepo kwa msongamano mkubwa wa wagonjwa katika hospitali nyingi mpya za Wilaya hali ambayo hupelekea wagonjwa kuchukua muda mrefu kupata huduma . Hivyo Kamati inaishauri Wizara kutoa elimu zaidi kwa wananchi pamoja na kuweka miongozo ambayo itawalazimu wananchi kufuata utaratibu wa kuanza matibabu kwa ngazi ya chini ili kuepusha msongamano huo.

v. Kamati imebaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalamu wa afya katika Hospitali na Vituo vya Afya Pemba miongoni mwa sababu hiyo ni kutokana na kuwa matangazo ya ajira yanayotolewa huanzia upande wa unguja hali inayopelekea wataalamu wengi wanaoomba nafasi za ajira kubakia unguja. Hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Nchi (OR) Shreia, utumishi na Utawala Bora inapotoa matangazo ya ajira ni vyema kuanzia Pemba ili kuiwezesha Wizara kuwa na wataalamu wa afya Pemba.

vi. Kamati inawashauri wafanyakazi katika taasisi za Umma kuwa na mashirikiano katika ufanyaji kazi wao ili kuboresha utoaji huduma bora kwa wananchi.

vii. Kamati inaielekeza Wizara kuhakikisha kuwa inafanya mapitio ya mara kwa mara katika vituo vya Afya pamoja na Hospitali ili kutatua changamoto zinazojitokeza katika vituo hivyo na kuondosha malalamiko kwa wananchi kwenye upataji wa Huduma bora za kimatibabu.

## 3.3.3.2 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA MICHEWENI PEMBA.

### 3.3.3.2.1 CHANGAMOTO

- Uhaba wa Wataalamu wakiwemo wa ICU, waliopo ni waliopewa

mafunzo ya dharura tu.

- Uchakavu wa Vipoza Hewa (AC) katika vyumba vya upasuaji na kupelekea kufanyiwa matengenezo kila mara.
- Hospitali haina store wala sehemu ya kuwekea maiti.
- Kukosekana kwa mafeni katika Sehemu ya mapokezi
- Mitaro kuziba  mara kwa mara.
- Umeme mdogo kunapelekea changamoto ya mifumo kutokufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa.

#### 3.3.3.2.2 USHAURI/ MAONI YA KAMATI.

1.Kamati inaishauri Wizara kuomba kibali Serikalini kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa fani mbali mbali ikiwemo wa ICU katika hospitali za Wilaya na Mikoa ili kuendeleza kazi nzuri wanayoisimamia ya kuwapatia wananchi Huduma bora za Afya.

i. Kamati inaishauri Wizara kuifanyia marekebisho milango ya vyumba vya upasuaji  na ICU ili iweze kuruhusu kuingia ndani wale wanaoruhusiwa tu.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia UPS yenye uwezo kulingana na mahitaji ya matumizi yaliopo Hospitalini hapo ili kuweka sawa umeme unapopungua au kuwa mkubwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za mifumo hospitalini hapo.

### 3.3.3.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA CHUMBUNI UNGUJA.

#### 3.3.3.3.1 CHANGAMOTO

- Ukosefu wa vipoza hewa (AC) katika vyumba vya dharura (Emargency).
- Upungufu wa wafanyakazi hasa wataalamu katika kitengo cha ICU.
- Uhaba wa nafasi katika sehemu ya kungojea wagonjwa (waiting Area) na kupelekea msongamano wagonjwa watoto na watu wazima.

#### 3.3.3.3.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

I. Kamati inaishauri Wizara kuweka vipoza hewa katika chumba cha ICU sambamba na kulifanyia maboresho jengo kwa kuweka japo mafeni sehemu zilizo na upungufu wa hewa.

II. Kamati inaishauri Wizara kuomba kibali Serikalini kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa fani mbali mbali ikiwemo wa ICU katika hospitali za Wilaya na Mikoa ili kuendeleza kazi nzuri wanayoisimamia ya kuwapatia wananchi Huduma bora za Afya.

III. Kamati inaishauri Wizara kupitia uongozi wa hospital kuweka utaratibu mzuri kuepusha mchanganyiko baina ya wagonjwa watoto na wagonjwa watu wazima ili kuwalinda watoto kutokana na udhaifu wa kinga zao kwenye maambukizi ya maradhi.

### 3.3.3.4 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA MWERA PONGWE UNGUJA.

#### 3.3.3.4.1 CHANGAMOTO:

- Kukosekana kwa kitanda cha kuokoa maisha ya mtoto (Radiant warm).
- Upungufu wa wafanyakazi na mtaalamu wa usingizi pamoja na Dathami mashine katika chumba cha wazazi.
- Ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi katika chumba cha kufulia.

#### 3.3.3.4.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inaishauri Wizara kuona ipo haja kwa Hospitali hii kuwapatia kifaa cha kuokoa maisha ya mtoto kwani ni muhimu sana kuwepo hospitalini hapo.
ii. Kamati inashauri Wizara kuengezea nguvu kazi pamoja na mtaalamu wa usingizi katika chumba cha wazazi sambamba na kuwapatia mashine ya dathami ili kuepusha vifo vya mama na watoto wachanga.
iii. Kamati inaishauri Wizara kupitia wasimamizi waliopewa dhamana ya kununua vifaa ili kuweza kukifanyia maboresho chumba cha kufulia kwa kuwapati vifaa vyote vinavostahiki ili kurahisisha utendaji kazi zao.
iv. Kamati inaishauri Wizara kufanya mazungumzo na mkandarsi ili aweze kuuongeza urefu uzio ambao umeizunguka Hospitali.

### 3.3.3.5 ZIARA YA KAMATI KATIKA HOSPITALI YA WILAYA IJITIMAI UNGUJA

#### 3.3.3.5.1 CHANGAMOTO

- Uhaba wa vifaa vya kutendea kazi kama vile Jokofu (Friji) la

kuhifadhia dawa sehemu ya madawa, Viti vya kubebea wagonjwa, vifaa vya mazoezi kwa ajili ya wagonjwa wa viungo.

- ❖ Ukosefu wa madaktari katika kitengo cha ICU
- ❖ Kutokufanyakazi kwa mfumo pamoja na uhaba wa vitendea kazi vya mfumo kama vile computer na mtandao wa uhakika.
- ❖ Katika ICU ya watoto Njiti kuna changamoto kubwa ya vitendea kazi na mfumo mzima wa utoaji huduma katika chumba hicho.
- ❖ Ukosefu wa Daktari dhamana katika jengo la mkono kwa mkono.
- ❖ Kuengezeka kwa wagonjwa wa clinic kutokana na clinic ya wazazi ya mnazi mmoja kuhamishiwa Hospitalin hapo.

**3.3.3.5.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.**

I. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia eneo la kutosha na vifaa vya mazoezi kwa wagonjwa ambao wanaenda katika clinic ya viungo sambamba na kuwaengezea ujuzi wataalamu wanaohudumia cliniki hiyo.

II. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia viti vya kubebea wagonjwa ili kurahisisha matibabu kwa wagonjwa wenye mahitaji maalumu.

III. Kamati inaishauri wizara kuimarisha miundombinu ya mtandao sambamba na kuwapatia computer za kutosha kwa ajili ya matumizi ya mfumo Hospitalini hapo.

IV. Kamati inaishauri Wizara kuomba kibali Serikalini kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa fani mbali mbali ikiwemo wa ICU katika hospitali za Wilaya na Mikoa ili kuendeleza kazi nzuri wanayoisimamia ya kuwapatia wananchi Huduma bora za Afya.

V. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia Daktari dhamana kitengo cha

Mkono kwa mkono ili kurahisisha ushulikiaji wa kesi za udhalilishaji hospitalini hapo .

VI. Kwa vile cliniki za mnazi mmoja zimehamishiwa hospitalini hapo, kamati inaishauri Wizara kuengeza Daktari pamoja na vitendea kazi kama Mabenchi ya kukalia wagonjwa.

VII. Kamati inaishauri Wizara kukifanyia maboresho makubwa chumba cha ICU ya watoto njiti kama ifuatavyo:-

- Kutokana ufinyu wa nafasi waengezewe eneo lililopo pembeni ambalo tayari limeshapimwa.
- Ipo haja ya kuongezwa idadi ya vitanda kwani vilivopo ni kidogo sana na mahitaji ni makubwa kama vile (Ressucitation Bed, Nicu bed) na;
- kuwekwa sink la kukoshea Mikono na mashine ya Pulse Oxymeter.

## 3.4 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103)

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, program imetenga Shilingi **39,883,789,000/=** sawa na asilimia **14** kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zilizopangwa katika programu hii, ambapo Shilingi **2,093,456,000/=** zitatumika kwa shughuli za uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, Shilingi **10,195,229,000/=** kwa ajili ya Utumishi na Uendeshaji, Shilingi **2,070,100,000/=** kwa ya Taasisi ya Utafiti. Aidha Wizara imetenga Shilingi **25,525,004,000/=** kwa ajili ya Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afya Pemba.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

ii. Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa sera, sheria, na miongozo ya utoaji huduma za afya;

iii. Kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa kugharamia huduma za afya;

iv. Kufanya tafiti, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma;

v. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya; na

vi. Kuimarisha miundombinu ya huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri.

Utekelezaji halisi wa Programu hii ni kama ifuatavyo:-

## 3.4 MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF)

Mfuko wa huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa rasmi kwa sheria Nam. 1 ya mwaka 2023. Dhana ya kuanzishwa kwa mfuko wa huduma za Afya Zanzibar inalenga kuwawezesha wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar kupata huduma bora za Afya kwa usawa na endelevu bila vikwazo vya kifedha.

### 3.4.1.1 CHANGAMOTO.

- ✓ Kuengezeka kwa mfumuko wa bei za vifaa tiba na dawa.
- ✓ Kuengezeka kwa wategemezi na kupungua kwa wachangiaji.

- ✓ Kuwa na idadi kubwa ya wanachama ambao wana umri mkubwa na hawachangii katika mfuko.
- ✓ Kutoongezeka kwa ukuaji wa uchumi kunaweza kupelekea kupungua kwa ajira na kupunguza michango ya wanachama.
- ✓ Kutokamilika kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar kuwa wanachama.
- ✓ Kuengezeka kwa vitendo vya udanganyifu kwa waajiri (kutoa taarifa zisizo sahihi za viwango vya mishahara), watoa huduma (kughushi madai ya huduma za afya yasiyo sahihi), wanachama (kutumia vibaya fursa ya matibabu bila ya mahitaji na kuruhusu kadi zao kutumiwa na wasiokua wanachama wa mfuko).
- ✓ Ukuaji mdogo wa ajira na mishahara.
- ✓ Ufuatiliaji usioridhisha wa kuwasimamia sekta binafsi kulipa mishahara elekezi iliyotolewa kwa mujibu wa viwango vya chini ya mishahara na serikali.
- ✓ Idadi ndogo ya wafanyakazi wa mfuko pamoja na haja ya kujengewa uwezo wa kusimamia uendeshaji wa mfuko.

### 3.4.1.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

*i.* Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na wataalamu wa mfuko ili kuweka mifumo imara ya utambuzi ili kuepusha udanganyifu sambamba na kuweka adhabu kali kwa wale watakaofanya udanganyifu kwenye kupata huduma.

*ii.* Kamati inaishauri wizara kupitia mfuko huu wa Bima ya Afya Zanzibar kuandaa utaratibu wa kuweka huduma za VIP kwa Hospital zinazojengwa za Mikoa ili kuwapa hadhi viongozi na wale watakaomudu gharama za huduma za VIP wakati wanapokwenda Hospiatali kupata matibabu kupitia mfuko huu.

*iii.* Kamati inaishauri Wizara kukaa uongozi wa mfuko wa huduma za Afya Zanzibar pamoja na wamiliki wa Hospitali Binafsi kuweza kutatua changamoto wanaozipata kwenye kutekeleza mfuko huu ikiwemo madai ya udanganyifu ya utoaji huduma na madai ya ucheleweshwaji wa malipo yao.

*iv.* Kamati inaishauri Wizara kupitia wataalamu wake wa Tehama kwa kushirikiana na wataalamu wa Mfuko kuboresha miundombinu ya mifumo ili mtu aweze kupata historia za taarifa za maradhi yake pamoja na dawa ambazo alishawahi kuzitumia kwa kutumia mifumo.

*v.* Kamati inaishauri Wizara kuwapatia Jengo la kudumu kwa ajili ya kuendeshea huduma za mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar ( ZHSF) ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

## 3.5 PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2)

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Shilingi 61,329,600,000/= zimepangwa kutumika kwa hospitali ya Mnazi Mmoja. Kati ya hizo Shilingi 23,069,600,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 15,260,000,000/=kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa hospitali zikiwemo huduma za uchunguzi na matibabu. Aidha, miradi ya maendeleo imepangiwa Shilingi 23,000,000,000/= kati ya fedha

hizo Shilingi 2,000,000,000/= kutoka Serikalini kwa ajili ya ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Shilingi 21,000,000,000 ni Mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo (BADEA, KUWAIT NA SAUDI FUND).

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

*(i)* Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa kwa mashirikiano na sekta binafsi pamoja na upatikanaji wa huduma za matibabu ya rufaa

*(ii)* Kuendelea kutoa huduma za kibingwa ikiwemo usafishaji damu kwa wagonjwa zikiwemo huduma za figo, uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya satarani (Chemotherapy), huduma za ubongo na uti wa mgongo.

*(iii)* Uimarishaji wa kambi maalum za matibabu na kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani

*(iv)* Kuratibu na kufanya tafiti za maradhi mbalimbali

*(v)* Kuongeza ajira kwa wataalamu wakiwemo wataalamu bingwa na wabobezi

*(vi)* Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa (Electronic Medical Record EMR); na

*(vii)* Kuanza ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia mradi wa BADEA, Saudi na Kuwait fund.

### 3.5.1 ZIARA YA KAMATI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO.

Wizara inaendelea na kutekeleza programu ya miradi ya maendeleo yenye jumla ya TZS 129.12 bilioni (TZS 75.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 56.11 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo).

Kamati katika kufuatilia utendaji kazi wa Wizara inayoisimamia ilifanya ziara ya kuikagua miradi 5 ambayo inaendelea na ukamilishwaji kwa lengo la kujionea mwenendo wa ujenzi na kupata changamoto za miradi hiyo ili kutoa ushauri ni jinsi gani wanaweza kuzitatua ili kupata miradi iliyo bora.

#### 3.5.1.1 MRADI WA KITUO CHA AFYA JADIDA :

Ujenzi wa kituo cha Afya Jadida ni mradi wa miezi 12 na utekelezaji wake ulianza rasmi tarehe 28 juni 2024 na unarajiwa kukamilika tarehe 28 Juni 2025. Mradi huu unajengwa kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa gharama ya Tsh. 3,883,011,270 na unasimamiwa na wakala wa majengo Zanzibar (ZBA). Mradi huu unajengwa na mkandarasi BENCHMARK ENGINEERING COMPANY LIMITED na mpaka sasa mradi umefikia asilimia 55 ya utekelezaji.

##### 3.5.1.1.1 CHANGAMOTO

Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

- Kukosekana kwa uzio eneo la mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya.
- Ucheleweshwaji wa malipo kwa mkandarasi.

##### 3.5.1.1.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.

i. Kamati inaiomba Serikali inapotekeleza Miradi mikubwa ya

Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika hasa kwenye michoro ili kuepusha changamoto ya matumizi yasiyotarajiwa ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mkataba wa awali.

ii. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kwenye miradi ya ujenzi kwanza kuanza kujengwa uzio kabla ya kuanza na ujenzi wa mradi ili kuepusha upotevu wa vifaa na mali ghafi za ujenzi huo sambamba na kuweka ulinzi katika uzio huo.

iii. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuwalipa kwa wakati wakandarasi kulingana na ukubwa wa kazi uliofanyika ili kurahisha kukalika kwa miradi ya maendeleo kwa muda uliyopangwa.

### 3.5.1.2 MRADI WA TANURI LA KUCHOMEA TAKA VITONGOJI PEMBA NA KIBELE UNGUJA.

Mradi wa Chomeo la taka ni mradi wa miezi 16 ambao umejengwa kwa Fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mkandarasi wa Waste Environmental and Land Surveying company limited (WELS CO LTD). Mradi huu una uwezo wa kuchoma taka kilogram 900 kwa Unguja na Kilogram 750 kwa Pemba kwa saa moja.

Miongoni mwa mafanikio ya mradi huu ni kutembelewa na taasisi mbali mbali kwa lengo la kujifunza na kuutangaza mradi huu.

### 3.5.1.2.1 CHANGAMOTO :

Licha ya nia njema ya serikali ya kuanzisha Mradi huu, kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

- Maeneo ya mradi hayana uzio.
- Mradi unachangamoto ya ukosefu wa maji
- Wafanyakazi wanaishi mbali na maeneo uliopo mradi.
- Kukatika kwa umeme mara kwa mara katika eneo la Mtambo.

### 3.5.1.2.2 USHAURI/MAONI /MAPENDEKEZO YA KAMATI.

i. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kwenye maeneo ya miradi hii Unguja na Pemba kunakuwepo uzio mkubwa sambamba na kuweka ulinzi madhubuti ili kuepusha uharibifu na upotevu wa vifaa vya mradi.

ii. Kamati inaishauri wizara juu ya uwezekano wa kulitatua tatizo la maji katika maeneo ya mradi huu kwa Unguja na Pemba, na ikiwewezekana kuwashiriisha Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili kusaidia kulitatua tatizo hili.

iii. Kamati inapendekeza kwa Wizara kuwatafutia usafiri wafanyakazi utakaoweza kuwachukua na kuwawahisha Kazini ili waweze kutekeleza kazi za mradi kwa wakati na ufanisi zaidi.

iv. Kamati inaishauri Wizara kununua Generator yenye uwezo kwa ajili ya kuendeshea mradi wa Vitongoji Pemba na Kibele kwa Unguja pindi inapotokezea umeme kuzimwa.

v. Kamati inaishauri Wizara kuweka magari maalumu kwa ajili ya kubebea taka

zinazotokana  na taka za Hospital na Vituo vya Afya ili kuepusha uharibifu wa mazingira.

vi. kamati inashauri wizara kuitangaza miradi hii kwa taasisi binafsi ili wapate kuitumia na kuengeza mapato Serikalini.

### 3.5.1.3 MRADI WA NYUMBA ZA WAFANYAKAZI VITONGOJI PEMBA NA MWERA PONGWE UNGUJA.

Katika kutekeleza kamati imepata fursa ya kutembelea Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba za wafanyakzi umekusudia kuimarisha utoaji wa huduma za uhakika na kwa wakati katika Hospitali za Wilaya. Kukamilika kwa mradi huu kutatoa fursa kwa wafanyakazi wa Afya kupata uhakika wa makaazi ya karibu, kuwapunguzia gharama na kuwaondolea usumbufu wa kusafiri masafa marefu. Sambamba na hilo Serikali itaweza kupunguza gharama kubwa za kuwafata majumbani madaktari hasa wakati wa usiku na siku za mapumziko inapotokezea dharura.

Kwa upande wa Nyumba ya Wafanyakazi Vitongoji; ni mradi wa mwaka mmoja ambao utekelezaji wake ulianza tarehe 22 juni 2024 na unatarajiwa kumalizika tarehe 25 juni 2025. Mradi huu unajengwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa gharama za Tsh. 4,086,243,250/-. Aidha, Mradi unasimamiwa na mshauri elekezi Mekon Arch Consult pamoja na Mkandarasi, KMKM Marine Engineering &General Trading Company Ltd (Main Contructor) kupitia (Sub Contructor) MJR Investment Co. Ltd.

**Kwa upande Nyumba ya wafanyakazi Mwera Pongwe;** Pia ni mradi wa mwaka mmoja (miezi 12) ambao utekelezaji wake ulianza tarehe  Januari 2024 na

unatarajiwa kukamilika Januari 2025. Mradi huu unajengwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibarkwa gharama ta Tsh. 3,808,081,582/-. Aidha, Mradi unasimamiwa na mshauri elekezi Mekon Arch Consult pamoja na Mkandarasimzawa Rans Company Limited.

**3.5.1.3.1 CHANGAMOTO :**

Kamati imebaini changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa miradi hii

- Ucheleweshwaji ya Malipo.
- Kuongezeka kwa gharama za ujenzi kulikotokana na kazi za ziada za ujenzi ambazo hazikuwemo kwenye mkataba wa awali ulisainiwa kabla ya mapitio ya mshauri elekezi kama vile ujenzi wa kazi za nje (land scaping), uzio wa nyumba (block fence), uwekaji wa lift, (eneo la kufulia) Laundry area, Electrical works na pumps house.
- Kuchelewa kumaliza kwa mradi kwa muda uliopangwa kutokana na kuengezeka kwa kazi za ziada.

**3.5.1.3.2 USHAURI/MAONI YA KAMATI.**

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika hasa kwenye michoro ili kuepusha changamoto ya matumizi yasiyopangwa ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mkataba waliokubaliana awali na pia kupelekea kuchelewa kumaliza kwa Miradi.
ii. Kamati inaisisitiza Serikali kupitia Wizara ya fedha kufanya malipo kwa wakati ili kuuwezesha mradi uweze kutekelezwa na kumalizika kwa wakati uliopangwa.

### 3.5.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA AFYA KWA UJUMLA

Ukiacha changamoto walizoziona kamati Katika Ziara mbali mbali kama tulivyoainisha, Wizara kwa ujumla wake pia inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Uingiaji usioridhisha wa fedha za kuendesha Hospitali na kupelekea huduma nyingi za hospitali kuzorota.
ii. Uchakavu na uhaba wa miundombinu ya vituo vya Afya ikiwemo majengo, mashine na vifaa tiba.
iii. Upungufu wa rasilimali watu katika kada mbali mbali za afya wakiwemo madaktari, wataalamu wa ganzi na usingizi, Wataalam wa ICU, wauguzi shahada ya kwanza, wakaguzi wa kemikali, wahandisi vifaa tiba n.k pamoja na watendaji wengi wa Hospitali kutokuwa na ujuzi wa kutosha kwenye taaluma zao.
iv. Kuwepo kwa uwezo mdogo wa baadhi ya watendaji katika kuibua na kusimamia miradi kutokana na kutokuwa na kitengo maalum cha wizara kinachosimamia utekelezaji wa miradi.
v. Kurejea na kuenea kwa kasi homa ya Malaria sambamba na kuengezeka kwa maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza yakiwemo maradhi ya shindikizo la damu na kisukari
vi. Ukosefu wa miundombinu ya TEHAMA hasa kwenye vituo vya afya.
vii. Kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha za ziada (variations) katika miradi mingi inayotekelezwa hali iliyopelekea Wizara kuwa na ongezeko kubwa la fedha katika miradi hiyo kinyume na Bajeti ya fedha za awali zilizopangwa.

viii. Kuwepo kwa vyanzo vichache vya mapato katika sekta ya afya lakini Kupangiwa kiwango kikubwa cha makusanyo yatokanayo na vyanzo vya mapato ya ndani kinyume na hali halisi ya vyanzo vya mapato vilivyopo hali inayopelekea kutokuwepo kwa ufanisi katika makusanyo wakati wa utekelezaji wa bajeti husika.

ix. Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa Hospital ya Wete.

x. Uelewa mdogo kwa wananchi na watoa huduma juu ya utumiaji wa huduma za mfuko wa huduma za Afya.

xi. Ofisi ya Mkemia wana Ukosefu wa vifaa vya kisasa ambavyo vitatumika kufanyia uchunguzi.

xii. Kuondoshwa kwa chuo kikuu cha Afya chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya.

xiii. Kukosa Posho kwa waratib Pemba ambao ni wasaidizi wa wakurugenzi kwa upande wa Pemba.

### 3.5.3 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha kwa wakati Wizara ya Afya kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yao kama walivyojipangia kwenye bajeti, kwani kuchelewa kupatikana kwa fedha hizo kunasababisha kuzorota kwa shughuli nyingi za uendeshaji wa hospitali pamoja na vituo vya afya.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inaongeza nguvu katika kuzifuatilia na kuzisimamia ipasavyo Kampuni zote Binafsi za (outsource) zilizoingia makubaliano ya kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kutoa baadhi ya huduma katika Hospitali za umma ili kuona

huduma hizo zinatolewa kwa ubora na ufanisi. Kamati imebaini kuwa Kamati za Wizara zilizoundwa kusimamia Kampuni za Outsource bado hazikujipanga vizuri katika kufanikisha kazi hiyo. Ipo haja kwa Wizara kuzijengea uwezo Kamati hizo ili ziweze kufanyakazi ya kuzikagua Kampuni zote za outsource na kuhakikisha kuwa zinatoa huduma bora za afya kwa wananchi.

iii. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kibali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini cha uajiri wa wafanyakazi wapya wa kada mbali mbali za afya kila inapohitajika ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa wataalamu na madaktari katika hospitali zetu.

iv. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuimarisha Mpango Mkakati wa muda mfupi na mrefu wa kuwasomesha na kuwaendeleza madaktari, wauguzi na wafanyakazi wengine waliopo katika hospitali zetu ili kuwaongezea ujuzi katika kazi zao na kuwa na wataalamu wa kutosha wanaokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknologia katika sekta ya afya.

v. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuweka miundombinu ya TEHAMA kwenye Vituo vyote vya Afya na Hospitali kwa Unguja na Pemba ili mifumo inayohusiana na taarifa sahihi za huduma za afya iweze kusomana katika vituo na Hospitali hizo.

**vi.** Kamati inaishauri wizara kuchukua juhudi zaidi katika utoaji wa Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar ambayo imeonekana kurejea kwa kasi samababamba na kutoa elimu kwa jamii juu namna bora ya kujikinga maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

vii. Kamati inaishauri Serikali inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika ili

kuepusha changamoto ya matumizi ya ziada ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mikataba ya awali na Wakandarasi pamoaja na kuchelewa kumaliza kwa miradi.

viii. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na Wafadhili wa ujenzi wa Hospitali ya Wete ili Hospitali hiyo ijengwe kwa mujibu wa Makubaliano.

ix. Kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha mfuko wa bima ya afya ambapo kamati inaisisitiza Wizara kusimamia vyema utendaji kazi wake kwa kuondoa changamoto zinazojitokeza baina ya mfuko na Hospital Binafsi sambamba na kutoa elimu kwa wananchi juu ya mfuko huu kwa ujumla.

x. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Wizara husika wakati wa kupanga mafungu ya Mapato ya Wizara pamoja na Taasisi zake zote zinazokusanya kupitia vyanzo vyake vya ndani ili kukadiria bajeti yenye uhalisia kwa mwaka husika na sio bajeti ya kufikirika.

xi. Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa kufanya ukarabati wa Vituo vya Afya 11 vya Daraja la Kwanza na kukamilisha Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Mkoa kwa lengo la kutoa huduma bora na za kisasa.

xii. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia ipasavyo ukamilikaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za watumishi katika Hospitali za Wilaya kwa Unguja na Pemba ili kuwaondoshea usumbufu watumishi wanaofanya kazi kwenye Hospitali hizo ambao wanaishi mbali na vituo vyao vya kazi.

xiii. Kamati inaiomba Serikali kukamilisha Mpango wa kuvirejesha Vyuo na Taasisi za kitaaluma katika Wizara zake husika ikiwemo Chuo cha

Afya Zanzibar baada vyuo na Taasisi hizo kutoleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi zake ndani ya Mfumo wa Ugatuzi.

xiv. Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia na kukamilika kwa baadhi ya miradi; hivyo kamati inaiagiza Wizara kuendeleza mashirikiano katika kukamilisha jukumu hili la kusimamia miradi iliyobakia kwa lengo la kuwapatia huduma bora ya Afya wananchi wa kisiwa cha Zanzibar.

xv. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango Kuwapatia Posho Waratibu Pemba kwani waratibu hao ndio wasaidizi wa wakurugenzi kwa upande wa Pemba.

xvi. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuiimarisha miundombinu ya utoaji huduma katika Ofisi ya Mkemia mkuu kwa kuwapatia vifaa vya kisasa ambavyo vitatumika maabara ili kuweze kufanyika huduma za uchunguzi na kudhibiti sumu.

## 3.6 HALI YA KIFEDHA KWA UJUMLA.

Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2024/2025 imekadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 282,756,472,000/= (Fungu HO1) na Shilingi 61,329,600,000/= kwa matumizi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu HO2).

Aidha, Wizara inakadiriwa kukusanya shilingi 3,719,683,000/= na shilingi 1,339,086,000/= kwa Hosptali ya Mnazi Mmoja.

### 3.6.1 MAPATO

Kwa kipindi cha mwezi Julai mpaka Disemba 2024, Wizara ilitarajiwa kukusanya jumla ya TZS. 1,119,920,750 ambapo hadi kufikia Disemba 2024 TZS 1,769,581,978 sawa na asilimia 158 zilikusanywa. Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja Tsh. 669,941,735 zilikadiriwa kukusanywa kwa

kipindi cha Julai hadi Disemba ambapo mpaka kufikia Disemba 2024 Tsh. 384,829,020 sawa na asilimia 57.4.

### 3.6.2 UPATIKANAJI NA MATUMIZI YA FEDHA

Kwa upande wa Wizara Jumla ya **TZS** 131,217,807,706. zilipangwa kutumika kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 ambapo hadi kufikia Disemba 2024 TZS 100,131,759,573 zilipatikana kwa ajili ya Mishahara na matumizi mengineyo ya Ofisi sawa na asilimia 76.31.

Aidha, Jumla ya TZS 34,846,613.00. Zilipangwa kutumika kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo hadi kufikia Disemba 2024 TZS 17,195,142.74 zilipatikana sawa na asilimia 49.3.

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni sekta ambayo inahusika na Maendeleo ya Jamii ambayo yanazingatia Usawa wa Kijinsia wa wananchi. Wizara ina dhamana ya kuhakikisha inainua hali za kijamii na kiuchumi kwa wanawake, sambamba na kulinda haki za wazee, watoto, na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kutoka jumuiya za kitaifa, kikanda na kimataifa, sekta binafsi na asasi za kiraia.

Utekelezaji wa shughuli za Wizara unazingatia mpangilio wa Programu Kuu tatu na Programu ndogo tatu kama ifuatavyo: -

i. Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii - PH0401
ii. Programu kuu ya Uratibu na Utawala - PH0402
    a. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji,
    b. Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti
    c. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ofisi Kuu Pemba
iii. Programu kuu ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto - PH0403

Shughuli za programu hizo hutekelezwa kupitia Idara zifuatavyo: -

1. Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee.

2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

4. Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

5. Ofisi Kuu Pemba.

Wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2050 ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), Agenda ya Afrika (2063) na kusimamia Sera ya Jinsia ya Zanzibar 2016, Sera ya Hifadhi ya Jamii 2014, Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2002, Sheria ya Mtoto Nambari 6 (2011) na Sheria ya Wazee Nambari 2 (2020).

## 4.1 UPATIKANAJI WA FEDHA

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 12,000,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 23,315,462,000 kati ya fedha hizo shilingi 9,959,836,000 ni matumizi ya kawaida zinazohusisha shilingi 3,888,989,999 za mishahara na shilingi 6,073,837,000 za matumizi mengineyo. Kati ya Fedha za matumizi mengineyo shilingi 4,384,201,000 ni kutoka SMZ, shilingi 1,189,636,000 zinatoka kwa Mshirika wa maendeleo UNICEF na shilingi 500,000,000 kwa ajili ya uratibu wa Usawa wa Kijinsia. Aidha fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 13,355,626,000 zinazojumuisha fedha kutoka Serikalini 4,500,000,000, Ruzuku za washirika wa maendeleo (UNWOMEN) shilingi 536,000,000, UNFPA 208,000,000 na shilingi 8,111,626,000, ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Jumla ya **TZS** 7,757,262,030.00 zilipangwa kutumika kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 ambapo hadi kufikia Disemba 2024 TZS 4,759,474,412.00 zilipatikana kwa ajili ya Mishahara na matumizi mengineyo ya Ofisi sawa na asilimia 61.4

## 4.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

## 4.3 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)

Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu zaidi kwa kuimarisha mifumo ya Hifadhi ya Jamii ili kupunguza kiwango cha umasikini hapa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imetenga shilingi 5,798,835,000 sawa na asimia 25 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii.

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hii ilifanya ziara mbali mbali Unguja, Pemba na Dar Es Salam kama ifuatavyo:

I. Ziara kutembelea familia zenye mazingira magumu zaidi:
II. kutembelea Mradi wa ukarabati wa nyumba za wazee Limbani Pemba na Sebleni Unguja;
III. kutembelea kituo cha kulelea Watoto Mazizini na vituo binafsi Pemba .

Lengo la ziara hizo ni kufahamu Changamoto na Mafanikio yaliyopo kama ifuatavyo;

### 4.3.1 CHANGAMOTO

I. Kamati imebaini kuwepo kwa familia za watu wenye mazingira magumu zaidi ambazo bado hazijatambuliwa rasmi.
II. Kamati imebaini kutolewa kwa kiwango kidogo mno cha fedha zinazotolewa na Wizara kusaidia familia hizo.
III. Kamati imebaini kuwepo kwa Makaazi mengi yasiyoridhisha kwa familia zenye mazingira magumu zaidi.
IV. Kuendelea kuibuka kwa kesi mbali mbali za udhalilishaji wa Watoto

V. Uhaba wa wafanyakazi wahudumu na wapishi katika nyumba za Wazee Limbani.

VI. Kuendelea kuwepo kwa utitiri wa nyumba zisizorasmi za kulelea Watoto.

**4.3.2 MAONI /USHAURI WA KAMATI.**

i. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukamilisha hatua ya kwanza ya Matengenezo ya majengo mawili pamoja na ukumbi katika makaazi ya wazee Sebleni, kazi ni nzuri na inaridhisha.

ii. Kamati inaishauri Wizara kusimamia ipasavyo ujenzi wa matengenezo ya makaazi ya wazee Limbani ili uweze kukamilika kwa wakati.

iii. Aidha kamati imeshauri wizara kuwapatia wazee walimu wa mazoezi sambamba na kuliendeleza eneo kwa kupanda miti mbali mbali.

iv. Kamati inaishauri Wizara kutoa posho la mazingira magumu kwa kila mwanafamilia angalau 30,000/- na sio kwa familia nzima.

v. Kamati inaishauri Serikali kuzitengea bajeti maalum familia zenye mazingira magumu zaidi na zenye watoto wenye ulemavu zaidi ya mmoja ili waweze kujikimu mahitaji yao.

vi. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwatumia masheha ili waweze kusaidia kuzifahamu familia hizo katika maeneo wanayoishi. Hatua hiyo itarahisishia Wizara kuzifahamu familia hizo na kuiwezesha Serikali kuzitambua rasmi na kuangalia namna bora ya kuzisadia.

vii. Kamati inaishauri Wizara kuongeza juhudi katika kufuatilia na kuzibaini nyumba zisizo rasmi za kulelea Watoto zilizoanzishwa kinyume na utaratibu na kuzifungia mara moja.

viii. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa inaratibu vyema huduma za Mpango wa Pencheni jamii kwa wazee. Ipo haja kwa Wizara

kuhakikisha kuwa wazee wapya ambao wametimia umri wa miaka 70 wanasajiliwa na kuondolewa wale wote waliofariki ili wazee hao waweze kupatiwa haki yao kwa mujibu wa utaratibu na sheria zilizopo.

## 4.4 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)

Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni Uratibu Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inatekeleza shughuli zake kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayo lenga jinsia, watoto na kuwawezesha wanawake wajasiriamali, kupinga Ukatili na Udhalilishaji pamoja kuwajengea uwezo Wanawake kuingia kwenye nafasi za Uongozi.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 wizara imetenga shilingi 2,392,112,000 sawa na asimia 10 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii.

Programu hii ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Huduma za uratibu wa mapambano ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.
ii. Huduma za maendeleo ya Jamii na
iii. Huduma ya Maendeleo ya Watoto.

### 4.4.1 ZIARA YA KAMATI DAR ES SALAAM

Ziara ya Kamati Dar Es Salam; Kujengewa uwezo wa kuielewa Programu Maalum ya miaka 5 (2021/22-2026) Tanzania kuhusu usimamizi wa masuala ya kijinsia katika Serikali (Generation Equality Programme.

#### 4.4.1.1 MAONI /USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI

i. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuielimisha jamii hasa walengwa wa matukio ya udhalilishaji wa Watoto na wanawake juu namna bora ya kujikinga na udhalilishaji huo ili kuweza kusaidia kupungua kuibuka na hatimae kuondoka kwa kesi mbali mbali za udhalilishaji wa Watoto na wanawake.

ii. Kamati inashauri wizara kuvipeleka vikundi vya wajasiriamali kwenda kujifunza Tanzania bara ili kuengeza ujuzi ya jinsi ya kuendeleza vikundi vyao na kupata maslahi zaidi.

### 4.4.2 ZIARA YA KAMATI KATIKA SHIRIKA LA SAVE THE CHILDREN

SAVE THE CHILDREN ni miongoni mwa Mashirika ya kimataifa ambalo linashughulikia masuala ya watoto pamoja na haki zao. Katika kutekeleza jukumu hili, Save the Children kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikiendesha miradi mbali mbali ambayo inalenga kuimarisha na kustawisha haki za watoto. Miradi hiyo ni kama ifuatayo:

i. Mradi wa Kuwalinda watoto.
ii. Mradi wa Makuzi ya maendeleo ya watoto pamoja na elimu ya lazima.
iii. Mradi wa Haki za watoto na miongozo yake.
iv. Matukio ya udhalilishaji kwa watoto.

#### 4.4.2.1 CHANGAMOTO

Shirika la Save the Children pamoja na mafanikio yaliyopo linakabiliwa na changamoto mbali mbali katika kusimamia masuala ya Watoto zikiwemo:

i. Watoto wenye Ulemavu bado hawajafikiwa kwa kiasi kikubwa na Shirika.
ii. Uhaba wa wafanyakazi.

iii. Miradi ya Shirika imefika katika baadhi ya maeneo tu ya Zanzibar na kuacha maeneo mengine ambayo pia yanakabiliwa na changamoto mbali mbali za udhalilishaji na kukosekana kwa haki za Watoto.

**iv.** Kuwepo kwa suala la Muhali kwa wahusika wa vitendo vya udhalilishaji wakati wa uendeshaji wa kesi hizo kwa Watoto jambo ambalo hupelekea kukosekana kwa ushahidi na kesi hizo kushindwa kuzingatiwa.

**v.** Shirika kubadilisha muelekeo wa ufadhili katika eneo la kulinda haki za Watoto baada ya Mradi kumalizika na kuanzisha ufadhili katika maeneo mengine kwa mujibu wa mahitahiya Washirika wa maendeleo.

### 4.4.2.2 MAONI/ USHAURI WA KAMATI.

i. Kamati inashauri Shirika la Save the Children kufika katika maeneo ya pwani ili kunusuru watoto wa ukanda wa Pwani kwani wao ndio waathirika wakubwa wa ajira kwa watoto na udhalilishaji.

ii. Kamati inashauri Save the Children kuangalia zaidi sehemu zenye uhitaji kufikiwa haraka na kuwapa elimu wazee kuhusu malezi ya watoto.

iii. Pia kamati inashauri Save the Children kuongeza ufadhili zaidi katika kuendesha Miradi yake ili iweze kuifikia Zanzibar nzima katika masuala ya udhalilishaji pamoja na malezi kwa watoto.

iv. Kamati inaishauri Save the Children kuendelea kutoa mafunzo au elimu kwa Watoto juu ya udhalilishaji na utumikishwaji kwa watoto.

v. Kamati inashauri save the Children kuendeleza ufadhili

### 4.4.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA VIKUNDI VYA KINA MAMA VINAVOSIMAMIWA NA MRADI WA TOKOMEZA.

Mradi huu umelenga zaidi katika kutoa mafunzo katika kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kina mama na watoto, na hivi sasa mradi huu unatekelezwa kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia ilifanikiwa kuvitembelea baadhi ya vikundi vya kina mama wanaoendesha mradi wa Kilimo cha Mwani na kugundua baadhi ya changamoto kama ifuatavyo;

#### 4.4.3.1 CHANGAMOTO.

i. Kukosekana kwa soko la Mwani, Mtaji na bei kuwa ndogo hali iliyopelekea baadhi ya vikundi kushindwa kuuza na hatimae kuufungia ndani.

ii. Kuwepo kwa umeme mdogo pamoja na kukosekana kwa kisima katika eneo la kazi na kusababisha wakati mwengine wateja kukosa huduma katika kikundi cha Tufahamiane.

iii. Kukosekana kwa Vitendea kazi visivyo na ubora na maeneo ya kufanyia kazi kwa kikundi cha Bismillahi Muungoni.

#### 4.4.3.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI

i. Kamati inaishauri Wizara kupitia Mradi wa TOKOMEZA unaosimamiwa na Programu ya UN Women kuendelea kusaidia vikundi vya kinamama vya kujiendeleza kiuchumi na kuepuka kukabiliana na udhalilishaji kwa kuwapatia Mitaji zaidi badala ya mafunzo pekee. Hali hiyo itawasaidia kinamama hao kuweza kuomba mikopo na kujikomboa kiuchumi.

ii. Kamati inaishauri wizara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na wizara husika kuwatafutia maeneo ya kuendesha shughuli za kilimo cha

mwani ili vikundi hivyo viweze kuwa na ya uhakika wa maeneo hayo kwa ajili ya kilimo hicho.

### 4.5 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)

Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu, ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Wizara Pemba. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imetenga shilingi 4,738,047,000 sawa na asimia 20 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii. Shilingi 3,888,989,000 kwa ajili ya mishahara, shilingi 8,992,763,000 sawa asilimia 39 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya matumizi ya ofisi unguja na shilingi 1,402,704,000 sawa na asilimia 6 ya bajeti ya wizara kwa uratibu na uendeshaji shughuli Pemba.

Wizara ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

1. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara;

ii. Kununua nyenzo pamoja na vifaa vya Wizara;

iii. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa watumishi pamoja na kuwapatia maslahi yao.

### 4.5.1 CHANGAMOTO

i. Kamati imebaini kuwa bado Wizara inaedelea kukaa katika jengo la kukodi na kusababisha matumizi makubwa ya fedha kwa kulipia jengo hilo.

ii. Bado wizara haijaweza kuzifikia familia zote zenye mazingira magumu Zaidi.

iii. Kuendelea kujitokeza wazee wenye changamoto ya vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi vinavyoonyesha umri mdogo kinyume na uhalisia.

iv. Upungufu wa vyombo vya usafiri ikizingatiwa wizara inauhitaji mkubwa wa kufuatilia wazee na watu wenye mazingira magumu zaidi.

### 4.5.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI.

i. Kamati imeridhishwa na hatua zilizofikiwa katika kuanza kutekeleza Mradi wa PAMOJA wa kukuza Usawa wa Kijinsia na kuwainua wanawake kichumi. Mradi huo ni matokeo ya mazungumzo kati ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Benki ya Dunia ambao utatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi maalum ya SMT na Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto ya SMZ.

   Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni mia moja sawa na Shilingi Bilioni mia moja ambazo ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Asilimia 87(USD87,000,000) sawa na shilingi Bilioni 226,200,000,000 ya fedha hizo zitatumika kwa upande wa Tanzania Bara na asilimia 13(13,000,000) sawa na shilingi Bilioni 33,800,000,000 zitatumika kwa upande wa Zanzibar.

ii. Kamati inaitaka Wizara kukamilisha mambo yote yaliyohitajika kukamilishwa katika utekelezaji wa Mradi wa PAMOJA ikiwemo kukamilisha; Muongozo wa utekelezaji wa Mradi, kuthibitisha Mpango kazi na Bajeti ya Mradi, kufungua Account ya Mradi pamoja kuthibitishwa kwa Timu ya utekelezaji ili Mradi huo uweze kuanza kwa wakati na kufikia lengo lililokusudiwa.

**iii.** Kamati inaishauri Wizara kuwashawishi Washirika wa maendeleo (Save the Children) kuendeleza muelekeo wa ufadhili wa Mradi katika eneo la kulinda haki za Watoto baada ya Mradi kumalizika na kuacha kuanzisha ufadhili katika maeneo mengine ambayo bado hayajafanyiwa utafiti kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

iv. Kamati inashauri wizara kufikiria kuwa na Mradi wa makaazi kwa ajili kuzisaidia familia zenye mazingira magumu zaidi ili na wao waweze kufarajika

v. Kamati inaishauri Wizara ya (OR) fedha na Mipango kuzipa kipaumbele wizara ambazo zinauhitaji Zaidi usafiri ili ziweze kufanya kazi zake kwa kufanisi Zaidi.

vi. Kamati inaishauri Wizara kuwasimamia ipasavyo Waratibu wa Ustawi wa Jamii katika Shehia kushirikiana na Masheha katika kufuatilia masuala ya jamii katika Shehia ili kuepuka kuibuka kwa migogoro mbali mbali ikiwemo migogoro ya ardhi.

vii. Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha Rasimu ya awali ya Sera ya Maendeleo ya Jamii. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kujitahidi kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Mtoto ili iweze kutumika. Sambamba na kukamilisha Kanuni inayoongoza uwepo kwa Vituo binafsi vya malezi ya Watoto. Kuwepo kwa nyenzo hizo kutasaidia kulinda haki za Watoto na kuondokana na kukiukwa kwa haki hizo.

viii. Kamati imeridhika na juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia. Inazipongeza Wizara ya Elimu na mafunzo ya amali na Wizara ya Maendeleo ya Jamiii kwa kuunda Kamati itakayotathmini na kutaribu namna ya kuondoa vitendo vya kikatili na udhalilishaji katika skuli za msingi na sekondari. Sambamba na kuweka utaratibu wa kutembelea madawati yanayosimamiwa na vyuo vikuu ili kuona namna Taasisi hizo za elimu ya juu zinavyosimamia kutokomeza vitendo vya kikatili na udhalilishaji katika Taasisi hizo.

ix. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi ambapo jumla ya watumishi 22 wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi na watumishi 3 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

# SEHEMU YA TANO

## 5.1 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.

Wizara hii ni miongoni mwa wizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Awamu ya Nane hivyo wizara hii imeundwa na sekta huu nne ambazo ndizo zinazo unda wizara ya habari vijana utamaduni na michezo na sekta yenyewe ni kama hizi zifuatazo: -

*(i)* Sekta ya Habari;

*(ii)* Sekta ya Vijana;

*(iii)* Sekta ya Utamaduni; na

*(iv)* Sekta ya Michezo.

### 5.1.1 SEKTA YA HABARI

*(a)* Idara ya Habari na Maelezo;

*(b)* Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC);

*(c)* Tume ya Utangazaji Zanzibar;

*(d)* Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZGPA);

*(e)* Kampuni ya Kuunganisha na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX);

*(f)* Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar.

### 5.1.2 SEKTA YA VIJANA

*(i)* Idara ya Maendeleo ya Vijana;

*(ii)* Baraza la Vijana Zanzibar.

### 5.1.3 SEKTA YA UTAMADUNI

*(i)* Idara ya Utamaduni;

*(ii)* Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni;

*(iii)* Baraza la Kiswahili (BAKIZA).

### 5.1.3 SEKTA YA MICHEZO

*(i)* Idara ya Michezo;

*(ii)* Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ);

*(iii)*Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

*(iv)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepanga kutekeleza Program Kuu (4) zifuatazo:

i. Programu kuu ya maendeleo ya habari, utangazaji na uchapaji-**PJ0301**
ii. Programu ya maendeleo ya vijana-**PJ0302**
iii. Programu ya maendeleo ya utamaduni, sanaa na michezo - **PJ0304**
iv. Programu ya uendeshaji na mipango katika sekta ya habari, vijana, utamaduni na michezo - **PJ0304**

## 5.2 UPATIKANAJI WA FEDHA

Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imeongezeka kwa bilioni 2,890,220,000/- sawa na asilimia 16 ya ongezeko la matumizi ya kazi za kawaida. Kutoka bilioni 17,661,930,000/- mwaka 2023/2024 hadi 20,552,150,000/- mwaka 2024/2025. Kwa miradi ya maendeleo ongezeko ni bilioni 35,945,928,000/- sawa na asilimia 105 Kutoka bilioni 34,278,054,000/- mwaka 2023/2024 hadi bilioni 70,223,982,000/- mwaka 2024/2025. Ongezeko hili ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bajeti ya kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

Kwa kipindi cha julai hadi Disembaa Jumla ya TZS 59,436,328,685.00 zilipangwa kutumika ambapo hadi kufikia Disemba 2024 TZS 65,614,252,697.00 zilipatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Ofisi

sawa na asilimia 110. Aidha wizara Ilipangiwa kukusanya jumla Tsh. 6,895,358,829 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2024, hadi kufikia Disemba 2024 Wizara imeweza kukusanya Tsh. 3,845,391.552 sawa na asilimia 56 ya makadirio.

## 5.3 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

Programu hii inaundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji. Shughuli kuu zinazotolewa ni Urushaji wa Vipindi na Matangazo, kupitia TV na Redio, Utoaji wa Taarifa, Picha, Makala, Filamu na Sinema, Utoaji wa Magazeti, Usambazaji wa Maudhui, Kudhibiti na Kusimamia Shughuli za Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji, Kusimamia Shughuli za Uchapaji pamoja na kudhibiti na kusimamia shughuli za Vituo vya Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Utangazaji.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Tanzania Shilingi 11,878,756,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Progaramu hii, Kamati imeweza kutemblea taasisi mbali mbali ili kufahamu mafanikio na changamoto na kuweza kuishauri Serikali kama ifuatavyo:

### 5.3.1 SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS)

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria Nambari 11 ya mwaka 2008. Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) linachapisha magazeti manne (4) ambayo ni gazeti la siku (Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki (Zanzibar

Mail na Zanspoti) na gazeti la Zanzibar Leo Jumapili ambalo hutolewa kila siku Jumapili. Magazeti haya husambazwa Zanzibar nzima na Mikoa 22 ya Tanzania Bara kwa lengo la kusambaza taarifa zenye kuelimisha kuhusu mambo mbali mbali ya nchi, burudani na michezo.

### 5.3.2 MRADI WA UJENZI WA OFISI ZA SHIRIKA LA MAGAZETI.

Mradi huu ni miongoni mwa Miradi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao bajeti yake imetengwa katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Mradi umeanza utekelezaji wake mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 8,398.8 ambapo hadi kufikia disemba 2024 mradi huu umefikia asilimia 48.

#### 5.3.2.1 CHANGAMOTO.

i. Malipo ya fedha za mradi yanachelewa kuingia.
ii. Kukosekana kwa mtambo wa kisasa unaopelekea shirika kutokufanya kazi zake kwa ufanisi.

#### 5.3.2.2 MAONI YA KAMATI/USHAURI WA KAMATI

i. Kamati inashauri Wizara ya Nchi (OR) Fedha na mipango kuharakisha uingizaji wa fedha za miradi ili miradi hiyo iweze kutekelezeka kwa wakati.

ii. Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya fedha na mipango iweze kutekeleza maagizo ya kukata deni kwa taasisi zinazo daiwa japo kwa asilimia kidogo ili shirika liweze kujiendesha pia kamati imeitaka Shirika kuendelea kujiimarisha kibiashara kwa kutumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Shirika.

iii. Kamati inaendelea kuiomba Serikali kuu kupitia Wizara kuendeleza jitihada za kulipatia Shirika mtambo wa uchapishaji wa Magazeti ili

kupunguza gharama za Uchapishaji pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

iv. Pia kamati imelitaka shirika kuendeleza ubunifu katika usambazaji wa magazeti kwa njia mbali mbali.

### 5.3.3 WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 12 ya mwaka 2018. Majukumu makuu ya Wakala ni kutoa huduma za uchapaji pamoja na uuzaji wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi. Wakala wa Uchapaji unasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na anaawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Uchapaji.

#### 5.3.3.1 CHANGAMOTO

i. Uchakavu wa jengo la Wakala
ii. Ukosefu wa ofisi ya Wakala Pemba
iii. Ukosefu wa ghala la bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia
iv. Uhaba wa Fedha na Mtaji wa kuendesha Shirika.
v. Uhaba wa mitambo ya kisasa ya uchapishaji
vi. Upungufu wa Wataalam na mafundi wa mitambo ya Shirika.

#### 5.3.3.2 MAONI/USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI.

i. Kamati inaishauri serikali kuikamilishia fedha za mradi wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi za Wakala ili ujenzi huo uweze kukamilika kwa wakati.
ii. Kamati inaishauri Wakala wa Uchapaji kukopa ili iweze kujiendesha.

iii. Kamati inaishauri Wakala wa Uchapaji kuwalinda na kuwaenzi wateja wake waliorudi ili wasije kuwapoteza tena kwa kuimarisha huduma.

iv. Kamati inashauri Wizara wawapatie mafunzo baadhi ya watendaji wa shirika kwa kuwapeleka nchi jirani ili kupata mafunzo na uzoefu ili waje wamudu kuitumia vizuri mitambo itakayoletwa.

v. Kamati inaishauri Serikali kuwapatia ghala la kudumu Wakala wa Uchapaji ili kuondokana na changamoto ya kuhifadhia vifaa vyao pindi vinaposhushwa Bandarini.

**5.3.4 SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA –ZBC**

Shirika la ZBC limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam.4 ya mwaka 2013.Kabla ya kuanzishwa kwa Sherai hiyo shirika hili lilianzishwa kwa Tamko la Rais (Presidential Decree), kwa hati ya kisheria nambari 111/2011.Baada ya kuanzishwa kwa sheria hiyo 2013, Shirika la ZBC likawa ni muunganisho wa Taasisi mbili ambazo ni Sauti ya Tanzania Zanzibar na Idara ya Televisheni (TVZ) ili kuifanya sekta ya Habari kwa Zanzibar kuwa ni chombo kimoja chenye nguvu.

**5.3.4.1 CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZBC**

i. Uhaba wa wafanya kazi katika kituo cha utangazaji cha ZBC TV.

ii. Uhaba wa vitendea kazi na mitambo ya kisasa kama vile setelight

iii. Kutokuwepo kwa uzio katika kituo cha ZBC Pemba

iv. Uhaba wa usafiri kwa Shirika.

v. Kuwepo kwa muundo ambao hautambui uwepo wa nafasi ya Mkurugenzi wa Kituo cha ZBC Dar es Salam hali inayopelekea kukosa stahili na haki zake nyengine kwa mujibu wa Sheria.

vi. Uwepo wa Sheria ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013 ya muda mrefu ambayo imeonekana kuhitaji marekebisho.

vii. Kuwepo kwa mahitaji ya mapitio ya Kanuni za Sheria ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013.

**5.3.4.2 MAONI /USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

a. Kamati inalipongeza Shirika la ZBC kwa kuwa na mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa kazi zake licha ya kuwa na changamoto mbali mbali inazozikabili shirika hilo.

b. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kuongeza nguvu katika ukarabati wa kituo cha utangazaji Dar Es Salam ili kituo hicho kiweze kuwa katika hali nzuri na kufanyakazi kwa ufanisiwakizingatia kupata jingo la kudumu kwa shirika Dar es Salaam.

c. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha uwepo wa Sheria mpya ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013 ambayo ni ya muda mrefu.

d. Kamati inaishauri serikali kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini kuwapatia kibali cha uwajiri kwa ZBC TV ili waweze kuwaajiri Wafanyakazi na waondokane na tatizo na uhaba wa wafanyakazi.

e. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya utumishi serikalini kukamilisha hatua zilizobaki marekebisho ya Mapendekezo ya Muundo mpya wa Shirika ili kuweza kutambua baadhi ya nafasi ambazo katika sheria hazikuwemo.

f. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha ufanywaji wa mapitio ya kuwa na Kanuni za Sheria ya ZBC

### 5.3.5 ZIARA YA KAMATI KITUO CHA RADIO ISTIQAMA PEMBA.

#### 5.3.5.1 CHANGAMOTO

i. Radio ilizima kwa muda kutokana na mtambo wake kuwa chakavu.

ii. Uhaba wa wafanyakazi pamoja na ufinyu wa nafasi katika ofisi zao

iii. Sheria ya utangazaji ina changamoto katika uchangiaji wake kwa vyombo vya habari binafsi.

#### 5.3.5.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI.

i. Kamati inasisiza wizara kuifanyia mapitio upya Sheria ya Utangaji Zanzibar kwani imeshakuwa muda mrefu sasa haijafanyiwa mapitio.

ii. Kamati inashauri wizara kuvisaidia vyombo vya habari hasa vya redio ambazo tumetembelea kwa upande wa Pemba ili ziweze kuendelea kutoa habari kwa wananchi.

iii. Kamati inashauri wizara kuunda vipindi maalum kwa redio na TV ili wananchi wapate kuelewa miradi inaondelea katika wizara yake na nje ya wizara inayofanywa na Serikali.

### 5.4 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo Zanzibar ambapo kupitia Programu hii, huduma mbali mbali hutolewa kama vile Ukaguzi wa Filamu na Sanaa za Maonesho, Uendelezaji wa Matumizi Sahihi ya Kiswahili, Kusajili na Kusimamia Hakimiliki, Ukuzaji na Uendelezaji wa

Michezo Zanzibar, Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa Pamoja na Usimamizi wa Vyama vya Michezo.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Tanzania Shilingi 69,216,860,000 /= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Progaramu hii imeweza kutemblea taasisi mbali mbali ili kufahamu mafanikio na changamoto na kuweza kuishauri Serikali kama ifuatavyo:

### 5.4.1 MRADI WA UJENZI WA NYUMBA YA SANAA

Mradi wa ujenzi wa Nyumba ya Sanaa unatekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 3.92/- Mradi unajumuisha ujenzi wa jengo lenye ghorofa tatu (G+3) na ununuzi wa samani na vifaa vya ofisi. Hatua ya utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 40.

#### 5.4.1.1 CHANGAMOTO

i. Kutopatikana kwa mali ghafi za ujenzi kwa wakati.
ii. Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za mradi.

#### 5.4.1.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI

1. Kamati imeshauri wizara kusaidia kupatikana kwa mali ghafi hizo ili mradi wa ujenzi uweze kutekelezwa kwa wakati.

### 5.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR

Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ) limeanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo, Nambari 5 ya mwaka 2010. Miongoni mwa majukumu

yake ya msingi ni kusajili na kusimamia vyama vya michezo pamoja na kukuza na kuendeleza michezo katika ngazi zote hapa Zanzibar.

Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria nambari 5 ya mwaka 2010 na miongoni mwa majukumu ya msingi  ni kusimamia vyama vya michezo vilivyosajiliwa pamoja na kukuza na kuendeleza mchezo katika ngazi zote hapa nchini. Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar linaongozwa na Katibu Mtendaji na lina jumla ya wafanyakazi 14 wakiwemo wanawake sita (6) na wanaume nane(8) kati ya hao Unguja kumi na moja (11) na Pemba watatu (3).

### 5.4.2.1 CHANGAMOTO

(a) Uhaba wa fedha  pamoja na kukosa bajeti kwa baraza la michezo

(b) Ufinyu na uchakavu wa Ofisi ya Baraza.

(c) Uhaba wa Vifaa vya michezo pamoja na walimu wa kufundishia

### 5.4.2.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inashauri wizara kuwatafutia vifaa vya michezo wana michezo ili tuweze kupata vipaji zaidi zanzibar.

(b) Kamati inashauri Baraza la Michezo kutafuta mafunzo kutoka nchi ambazo zimeendelea kimichezo ili na sisi tupate uzoefu na kufanikiwa katika sekta hii.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuliongezea bajeti Baraza la Michezo la Taifa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza pamoja uendeshaji wa shughuli za Michezo kwani hivi sasa Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza vyema majukumu yake.

(d) Kamati inashauri wizara kuvipa mafunzo au semina vyama vya michezo hata nje ya nchi ili viweze kujiendesha wenyewe.

### 5.4.3 ZIARA YA KAMATI KATIKA MRADI WA UKARABATI WA UWANJA WA AMAANI NA GOMBANI AWAMU YA PILI

#### 5.4.3.1 UWANJA WA AMAANI

Mradi wa ukarabati wa Uwanja wa Amaan awamu ya pili unatekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 18.75. Mradi unajumuisha shughuli mbali mbali zikiwemo uondoaji wa nyasi bandia na uwekaji wa nyasi za Hybrid, ujenzi wa ukumbi wa mikutano, ujenzi wa miundombinu ya utangazaji na mawasiliano, ukarabati wa hoteli, na ujenzi wa mkahawa.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2024 jumla ya shilingi bilioni 2.25 zimelipwa kwa mkandarasi. Aidha, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 85.

#### 5.4.3.2 UWANJA WA GOMBANI - PEMBA.

Mradi wa ukarabati wa uwanja wa Gombani awamu ya pili unatekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 11. Mradi unajumuisha shughuli mbali mbali ikiwemo ujenzi wa paa, uwekaji wa viti vya watazamaji, ujenzi wa VIP ya watazamaji, ukarabati wa vyumba vya VIP, Ukarabati wa vyumba vya wachezaji, ujenzi wa eneo la kuegesha magari na ujenzi wa uzio.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2024 jumla ya shilingi bilioni 1.26 zimelipwa kwa mkandarasi. Aidha, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 54.

### 5.4.3.3 CHANGAMOTO ZA MRADI WA UKARABATI UWANJA WA AMANI NA GOMBANI

i. Magari yanayoingia kwa ajili ya mategenezo yanaharibu tatan katika kiwanja.

ii. Uwanja kufanyiwa ukarabati mara kwa mara kutokana na kutumika kwa shughuli zisizo za michezo zikiwemo kufanyika kwa gwaride katika sherehe za kitaifa.

iii. Sehemu nyingi za viwanja zimekosa au hazina miundombinu rafiki ya watu wenye uelemavu

iv. Ukumbi wa mchezo wa judo na ngumi bado hakuna vipoza hewa.

v. Kuchelewa kufika kwa vifaa vya kumalizia miradi hiyo.

### 5.4.3.4 MAONI YA KAMATI/USHAURI KWA UWANJA WA AMANI NA GOMBANI.

a) Kamati inaishauri wizara kuzidi kuimarisha utunzaji wa viwanja vya michezo vya Amani Complex na Gombani ili Zanzibar kuweze kufanyika mashindano ya michezo katika medali ya kimataifa.

b) Kamati inashauri wizara kuangalia namna bora ya kuweza kuviendesha viwanja vya michezo kiulinzi na kiusalama pamoja na kutunza miundombinu iliyopo katika maeneo hayo.

c) Kamati inashauri Wizara kupitia serikali kujenga viwanja maalum vitakavyotumika kwa ajili ya gwaride wakati wa Sherehe za kitafa ipo haja ya

Wizara kujifunza katika nchi nyengine ambazo zimejenga viwanja kwa ajili ya sherehe za kitaifa.

d) Kamati inashauri wizara ya habari kuwazingatia watu wenye mahitaji maalum katika Miradi hii ya viwanja ili na wao waweze kuvitumia na kujisikia kama wanathaminiwa na serikali yao.
e) Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuingiza kwa wakati fedha za miradi ili iweze kumaliza kwa wakati uliopangwa.
f) Kamati inashauri wizara kuwaongezea uwezo wafanyakazi wake ili waweze kujifunza namna ya kutunza viwanja hivyo pamoja na kuweza kuajirika katika Hoteli zilizopo katika Uwanja wa Amani.
g) Kamati inashauri wizara ya Habari kuliendeleza eneo la uwanja wa Gombani kwa kujenga hoteli ya kisasa ili kuendana na hadhi ya kiwanja kilichopo.

### 5.4.4 MRADI WA UJENZI WA VIWANJA VYA WILAYA NA MIKOA.

Mradi wa ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa unatekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 16 kuanzia Septemba, 2024 na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 134.00/- kwa malipo ya mkandarasi ambazo zitalipwa kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2024/25 hadi mwaka wa fedha 2028/2029, na shilingi bilioni 1.9/- kwa malipo ya mshauri elekezi.

Mradi unajumuisha ujenzi wa Viwanja 17 vya Michezo katika ngazi ya Wilaya na Mikoa Unguja na Pemba sambamba na complex ya maisara na kiwanja cha soka la ufukweni kitakachojengwa katika eneo la Maruhubi Zanzibar. Katika hatua ya awali viwanja vilivyoanza kujengwa ni Comlex ya Maisara, Kilimani Brizy, Kitope na Gombani Chake chake Pemba. Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2024 jumla

ya shilingi bilioni 21.2 zimelipwa sawa na asilimia 15.8 kwa malipo ya mkandarasi na shilingi milioni 785.6/- kwa malipo ya Mshauri elekezi ambazo zililipwa katika robo ya kwanza.

#### 5.4.4.1 CHANGAMOTO

i. Kiwanja kinachojengwa Mchanga Mdogo kisogezwe mbele Zaidi kutokana na eneo lipo karibu na skuli.
ii. Kuchelewa kuanza kwa Mradi, ambapo Mradi huo ulitakiwa kuanza mwaka 2022/23 lakini umechelewa kutokana na kutokamilika taratibu za kitaalamu za ujenzi.
iii. Baadhi ya miradi ya viwanja hivi haina uzio.

#### 5.4.4.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI

i. Kamati inampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kasi mpya na kubwa ya Miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo Unguja na Pemba.
ii. Kamati inaipongeza Serikali na inaunga mkono juhudi za serikali katika kufanya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya michezo unaoendelea nchini.
iii. Kamati inashauri wizara au mkandarasi wa viwanja vya michezo vilivyo karibu na skuli visogezwe mbele Zaidi kwa vile nafasi ipo ili kuepuka usubufu kwa wanafunzi wakati wa masomo.
iv. Pia kamati inashauri wizara kukijengea uzio kiwanja cha Mchangamdogo ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza kwa wananchi.
v. Kamati inashauri wizara kuwatumia washauri elekezi wazalendo ili kuepuka kuipa Serikali hasara katika miradi yake.

vi. Kamati inaishauri Wizara kuviezeka viwanja vya Wilaya ili viweze kutumika kwa ajili ya matumizi mengine ya kimichezo ikiwemo michezo ya kimataifa.

vii. Kamati inashauri wizara kuusimamia vizuri ujenzi wa viwanja vya michezo kwa vile muda wa ujenzi ni mchache ili viwe vyenye viwango na ubora.

## 5.5 PROGARAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA (PJ0302)

Lengo kuu la Programu hii ni kuratibu shghuli za maendeleo ya vijana, kuwawezesha kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia progaramu mbali mbali.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Tanzania shilingi bilioni 5,662,714,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### 5.5.1 CHANGAMOTO

i. Vitendea kazi vingi vinavyotumika katika miradi ya kuwajengea uwezo vijana ni vya zamani na havikidhi haja iliyokusudiwa.

ii. Vijana wengi hawajafikiwa katika kuwashirikisha katika miradi ya vijana kutokana na umbali wa maeneo hasa waliyopo Mkoa wa Kusini Pemba.

iii. Walimu waliyopo vituo vya kuwaendeleza vijana sio wa kudumu ni wa kuazimwa kutoka Vyuo mbali mbali kama Chuo cha Kilimo na kadhalika.

iv. Uhaba wa fedha za kuendeshea vituo vya kuwaendeleza vijana kiuchumi katika miradi mbali mbali .

v. Miundo mbinu ya Barabara ya kuelekea Chuo cha vijana Weni ni mbovu.

### 5.5.2 MAONI/USHAURI WA KAMATI

i. Kamati inashauri Wajumbe waliyopo Pemba kuwashajihisha wananchi au vijana kujiunga na chuo cha kuwaendeleza vijana Weni
ii. Kamati inashauri Wizara kuongeza fani za technolojia ili vijana waweze kupata ujuzi Zaidi na kuingia katika soko la ajira.
iii. Kamati inaishauri wizara ya Habari kuimarisha mipango yake ya muda mrefu na muda mfupi ya kuwajengea uwezo wa kitaaluma watendaji wake ili waweze kuwa na watendaji wenye katika fani mbali mbali na kuleta ufanisi katika kazi zao.
iv. Kamati inashauri wizara kuweza kuangalia namana ya kukiendeleza kituo cha vijana Kangagani  ili kiweze kufanya kazi.

### 5.6 PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA (PJ0304)

Kiujumla utekelezaji wa Programu Kuu hii unajumuisha Programu Ndogo Tatu nazo ni Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti, Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji na Programu Ndogo ya Uratibu wa Wizara Ofisi Kuu Pemba.

### 5.6.1 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

1. Changamoto ya ofisi kwa wafanyakazi baadhi ya taasisi zinamrundikano mkubwa wa watendaji jambo ambalo halileti ufanisi katika utendaji wa kazi.

2. Vyama vya michezo kushindwa kujiendesha vyenyewe na hivyo kuitegemea Wizara kwa asilimia mia moja.
3. Uchache wa vyombo vya usafiri kwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara, jambo ambalo linapelekea kushindwa kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji wa kazi za ofisi.

### 5.6.2 MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

a. Kamati inampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha sekta ya Michezo kupitia ujenzi wa Miradi mikubwa ya ujenzi wa Viwanja vya Amani na Gombani pamoja na viwanja vyengine vidogo vidogo.
b. Kamati inashauri wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kujenga nyumba ya Sanaa kwa upange wa Pemba ili wananchi wa Pemba nao waweze kuzitumia fursa hizo kuendeleza vipaji vyao vya kisanii katika fani mbali mbali.
c. Kamati inashauri wizara Nchi (OR) Fedha na Mipango kuwapatia fedha za miradi ilizopangwa kutumika katika miradi ili miradi iweze kutekelezeka kwa wakati.

## 6.0 HITIMISHO

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote Nne zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi zote pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati inapokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake. Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamadi Haji pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2024/2025.

Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata. Mwisho kabisa na kwa umuhimu mkubwa Kamati inawapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025.